# Nipashe

Jumatatu Machi 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581241

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US







**Dola** zaadimika Kenya, Tanzania yawa kimbilio wafanyabiashara

UKURASA 3




UKURASA 11

## Akodi muuaji kumuua baba yake mzazi

UKURASA 8

# Samia: Wapinzani wananipa changamoto nitimize majukumu

• **Mbowe** asema Rais Samia atashiriki mkutano wa CHADEMA... *Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akimbeba mtoto Zaujia Swalehe (1) baada ya kuzungumza na wananchi wa Usa River mkoani Arusha jana. **PICHA: IKULU**

## Mifuko ya mchanga yakutwa ghala la mbolea ya ruzuku

UKURASA 3


SPECIAL SUPPLEMENT ON COMPLETION OF TWO YEARS UNDER THE ABLE LEADERSHIP OF



HER EXCELLENCY DR. SAMIA SULUHU HASSAN

The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the achievements of the Government under the leadership of President **Dr. Samia Suluhu Hassan**

20th March 2023

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Congratulatory messages, Advertorials** and **Advertisements.**

The Guardian Nipashe

TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON +255 677 020 701

617309101

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com


MICHEZO YANGA YAIANDALIA BAMAKO DOZI NENE UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Maofisa wa Benki ya Tanzania Commercial Plc wakiongozwa na Ofisa Masoko, Dorothea Lymo, wakiwa pamoja na uongozi wa Shule ya Msingi Bunju B kitengo cha watoto wenye ulemavu wa akili walipotembelea shule hiyo jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa msaada wa vyakula na mahitaji mbalimbali ya kibinadamu kwa watoto hao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia: Wapinzani wananipa changamoto nitimize wajibu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema siasa sio uadui na anawachukulia wapinzani kama watu wanaompa changamoto ili atimize wajibu wake ipasavyo.

Rais alitoa kauli hiyo jana aliposimama kwenye mji wa Usa River mkoani Arusha kuwasalimia wananchi wa eneo hilo na kuwaruhusu wabunge wa mkoa huo kuzungumza, huku akiwataka mawaziri waliokuwapo kujibu hoja.

"Kwenye siasa tuko vizuri sana. Nadhani lile tendo la juzi la mtu wao (Godbless Lema) kurudi nchini na hakuna kilichotokea inaonyesha siasa zetu ziko imara sana," alisema.

Rais Samia alisema Mtanzania yeyote mwenye chama chochote cha siasa, anatofautishwa na mawazo na fikra.

"Mimi sichukulii wapinzani kama maadui, ninawachukulia kama watu watakaonionyesha changamoto zilipo nizitekeleze ili CCM iimarike. Mdogo wangu (Lema) aliniambia 'mama nataka kurudi' nikamwambia 'rudi', kasema 'mama nina kesi', nikasema 'nazifuta'. Amerudi tuimarishe siasa.

"Mwanaume ni yule anayejiamini, mwanamke ni yule anayejiamini, kwenye uwanja wa siasa tunajiamini, tuko vizuri na tutakwenda vizuri."

"Ninawashukuru sana, nawashukuru watoto wangu wa bodaboda, bodaboda mpooo? (wakaitikia tupoooo), wamenisindikiza kutoka mjini mpaka hapa mwendo ni huo mpaka 2025, ninawatambua," alisema.

**MAENEO YA UTAWALA**

Rais Samia alisema serikali haitarajii kuongeza maeneo mapya ya utawala kwa kuwa ni gharama kwenye utawala na kunyima fedha kwenda kwa wananchi katika huduma mbalimbali.

Alisema nchi iko vyema kiuchumi, maendeleo ya watu hasa kwenye elimu, maji na afya na kwamba uimarishaji wa miundombinu ili wananchi wapate huduma.

Rais alitoa ufafanuzi huo baada ya Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, John Pallagyo, aliyemwomba mji wa Mamlaka ya Mji Mdogo miaka 13 iliyopita na hakuna barabara ya kilomita moja jambo ambalo sio sahihi.

"Tiba ya haya yote ni kuupandisha hadhi uwe mji mdogo ili kutatua changamoto zilizoko," alisema.

Rais Samia alisema kuhusu upanuzi wa Uwanja wa Ndege Arusha, serikali imeshakamilisha tathmini na wananchi waliovamia eneo la jirani na uwanja wa ndege kwasababu walishajenga nyumba za kuishi watalipwa zaidi ya Sh. bilioni 11.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema Wilaya ya Meru ni ya uzalishaji na kwamba changamoto ya mashamba saba ikiwamo ya Kil Flora, wiki mbili zilizopita walikuwa na mawaziri na maofisa wengine.

Alitoa ufafanuzi huo baada ya baadhi ya wananchi wakiwa na bango lenye ujumbe wa kumwomba aingilie kati ili walipwe stahiki zao.

"Mashamba yote serikali iliyachukua ambayo walipewa mkopo kupitia Benki ya TIB kupitia dhamana ya serikali na hawakuwekeza, yatarudishwa Wizara ya Kilimo na yatatangazwa kwa ajili ya kuanza uzalishaji.

"Kati ya saba, matano yana kesi mahakamani, mawili hayana mojawapo la Kil Flora, wafanyakazi wanadai Sh. bilioni 3.4, tutakaa na Hazina ikibidi Wizara ya Kilimo wataweka fedha kwenye bajeti ili walipwe waondoke halafu serikali itashughulika na mmiliki."

Bashe alisema shamba lingine wizara imepewa ekari 3,000 na wamekubaliana na mkoa kuwagawia wananchi, ili wazalishe mazao ya mboga na matunda.

"Leo tumewakamata viongozi fulani huko Babati wakishirikiana na baadhi ya watumishi wa NFRA wakihujumu mahindi. Mfanyabiashara yeyote atakayebainika kanunua mahindi hayo atakamatwa na yatataifishwa," alifafanua.

**PATA MKOPO KWA HARAKA**

PATA MKOPO KWA HARAKA
HADI 200,000,000/=
KUTOKA
ENTERPRISE FINANCE LIMITED
KWAAJILI YA DHARURA
MBALIMBALI KAMA KULIPA
KODI YA NYUMBA,
KUNUNUA GARI,
KUBORESHA BIASHARA N.K

TUNAPATIKANA
DAR ES SALAAM 0677111333
NA ARUSHA 0677226960.

# ... kushiriki kongamano lililoandaliwa na CHADEMA

**Na Waandishi Wetu,**
ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, mwaka huu, ambako atazungumza na Watanzania kupitia Kongamano la Kitaifa lililoandaliwa na Baraza la Wanawake wa CHADEMA Taifa (BAWACHA) mjini Moshi.

Jana Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akizungumza na vyombo vya habari jijini Arusha, alisema kwa namna walivyofanya kazi na Rais Samia, wameamua kumwalika na yeye amekubali kuhudhuria kongamano hilo ili asikilize kinamama wa CHADEMA na upinzani wanavyosema.

"Siku zote anaongea na kinamama wa chama chake, leo tumemwalika aje asikilize, awaone, atambue kinachofanywa na kinamama wa CHADEMA, na mimi nitakuwapo kumpokea," alisema Mbowe.

Aliongeza: "Nimefurahi kwamba amekubali kuja kusikiliza changamoto. Huo nao ni ujasiri, kwa sababu yeye ni kiongozi wa serikali, Rais ni kiongozi wa serikali, ana haki ya kuwahudumia wananchi wote wa vyama vyote. Hatuamini kama atakuja kufanya siasa pale. Atakuja kutekeleza wajibu wake kama Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Taifa letu."

Katika mkutano huo, Mbowe alisema wao kama CHADEMA, watampokea, watamkaribisha na watamweleza changamoto na kwamba kazi hiyo itafanywa na kinamama ambao ndio watakaomweleza changamoto rasmi za chama chao, siasa za upinzani na taifa.

**WAKUTANA IKULU**

Kuhusu maridhiano, Mbowe alisema kuwa jana majira ya saa nne asubuhi, alikutana na Rais Samia Ikulu ndogo ya Serikali Mkoa wa Arusha ambako walizungumza mambo kadhaa.

"Tumekutana na kufanya kikao tukitambua kwamba miezi 12 iliyopita tulizungumza tena nilipotoka gerezani. Na katika kikao tulichokaa na Mheshimiwa Rais, tarehe 4/3/2022, tulikubaliana kujenga 'narrative' (simulizi) ya haki katika taifa.

"Haki kwenye demokrasia, haki kwenye uhuru wa watu, haki kwenye mahakama na mambo yote yanayohusu maisha ya binadamu. Kwa hiyo, tumekutana mwaka mmoja baadaye, japo tumekutana hapo katikati ku-review (kupitia) yale tuliyoyazungumza miezi 12 iliyopita kama viongozi wakuu wa vyama vikuu vya siasa katika nchi yetu, tumeishi yale tuliyokuwa tumekubaliana ama tumekuwa tunaviziana.

"Ninafarijika kusema kwamba tumefanya wote mwendo lakini hatujakamilisha kazi. Bado kuna kazi kubwa ya kufanya kurejesha taifa katika uhuru wake katika demokrasia ya kweli katika nchi na katika kusukuma maendeleo ya watu.

"Kwa hiyo, tumekubaliana na Mheshimiwa Rais kwamba tuendeleze maridhiano yetu na nimemwambia Mheshimiwa Rais kwamba mambo haya hayapaswi kwenda kwa mwendo wa konokono," alisema.

Mbowe alisema mambo hayo yanapaswa kupelekwa kasi, ili kupata mabadiliko stahiki katika katiba na sheria mbalimbali, ikiwamo mifumo na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ili kuhakikisha kile alichokiita uchafuzi uliofanyika mwaka 2019 na mwaka 2020 haujitokezi tena katika maisha ya Watanzania.

"Maridhiano hayajawahi kuwa kazi nyepesi, ni kazi ambayo inahitaji subira, inahitaji busara, inahitaji akili. Tumekuwa tuna tofauti kubwa sana kati ya sisi (CHADEMA) na CCM, hasa katika awamu iliyopita ya uongozi lakini tumejaribu kuziba nafasi.

"Bado kuna matatizo mengi na maridhiano hayamaanishi kwamba sisi kama CHADEMA, eti kwa sababu tunazungumza na Rais au Waziri Mkuu na serikali tutarudisha wajibu wetu wa kuisimamia na kuishauri serikali, hapana!

"Tutaendeleza kazi yetu ya upinzani kwa nguvu zote na hatutaogopa kuikosoa serikali, hatutaona haya kueleza sera mbadala katika taifa hili na sisi nia yetu ya kutaka kuingia madarakani iko palepale. Kwa hiyo, maridhiano hayaondoi dhamira yetu ya kuing'oa CCM madarakani.

"Hatuko hapa kuisaidia serikali irekebishe kama alivyosema mama (Rais Samia) iweze kufanya vizuri zaidi. Sawa, wao wafanye vizuri, lakini sisi tuna hakika tuna uwezo wa kufanya vizuri zaidi kwa sababu tayari wameshashindwa wao kwa zaidi ya miaka 60," alisema.

**RUZUKU**

Alipoulizwa kuhusu ruzuku wanayopaswa kuichukua, Mbowe alielekeza suala hilo litolewe ufafanuzi na Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje, John Mrema, ambaye alisema jambo hilo litajibiwa na Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika muda wowote kuanzia wiki hii kwa kuwa ndio mtendaji mkuu wa chama.

***Imeandaliwa na Godfrey Mushi na Tumaini Mafie (ARUSHA).**

HABARI KITAIFA

# Mifuko 776 ya mchanga yakutwa ghala la mbolea

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Kilimo, Hussen Bashe ameagiza kwa njia ya simu kukamatwa na kuhojiwa watumishi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) kutokana na kubainika mifuko 776 ya mchanga kwenye ghala, ikidaiwa kutumika kuchakachua mbolea.

Bashe alitoa agizo hilo alipozungumza na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, aliyekuwa ameongozana na kamati ya ulinzi na usalama na kamati ya siasa mkoani humo kukagua ghala la kuhifadhia mbolea ya Minjingu.

Aliagiza kukamatwa kwa Meneja wa Kanda Nyanda za Juu Kusini wa TFRA, Michael Sanga, Ofisa Masoko wa Kampuni ya Mbolea ya Minjingu, Mshindo Msola na msimamizi wa ghala la mbolea ya Minjingu mkoani humo.

Alisema tukio hilo ni hujuma ambayo haivumiliki na atahakikisha waliohusika wanachukuliwa hatua za kisheria.

"Mheshimiwa waziri tumekuja sasa baada ya kikao cha ndani mimi na kamati ya ulinzi na usalama, kamati ya siasa na watu wa TFRA kanda na Msola ambaye ni msimamizi tumekuja tumekuta mifuko 776 ambayo yote ni ya mchanga haijaandikwa ruzuku, lakini ni mifuko ile ile yenye chapa ya Minjingu na mifuko mingine, lakini TFRA wamesema Februari 24, mwaka huu, walipiga faini Sh. milioni 30 Februari 24 na mifuko ile ilibaki humu ndani," Mtaka alimweleza Bashe.

Baada ya maelezo hayo Waziri Bashe alisema hakuwa na taarifa ya ulipaji faini. "Mimi kama waziri kwanza sina hiyo taarifa ndio umenipa jana ulivyonieleza wamempiga faini bila ya mimi kufahamu, kwa hiyo huyo mtu wa NFRA aliyekuja hapo kuchukua sampo na kujiridhisha mchukueni mwekeni ndani atoe taarifa," alisema.

"Watu hao wa Minjingu wachukueni wawekeni ndani watoe maelezo ili kufanyike uchunguzi na mimi nitatoa taarifa kuhusu hili tatizo kwa sababu haiwezekani kwamba kuwe na mifuko ya michanga hatujui wakulima wangapi wamepewa mifuko ya michanga."

Pia, aliagiza kuangaliwa kwenye mfumo idadi ya wakulima wa Mkoa wa Njombe waliotumia mbolea ya Minjingu.

Akizungumza mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, kujibu hoja zilizoibuliwa na wabunge na wananchi wa eneo la Usa River, mkoani Arusha, Bashe alisema:

"Ndani ya ghala la kuweka mbolea, humo humo kaweka mchanga, nimeagiza wamkamate mwenye kiwanda, mwakilishi wake, wafunge ghala. Huu ni uhujumu uchumi, nimeagiza kampuni hii ruzuku yake tunaisimamisha huku tunafanya uchunguzi na kufuatilia wakulima wote nchi nzima walionunua mbolea hii."

"Inasikitisha sana mawakala tunawalipa haki zao wakileta madai hadi sasa tumelipa Sh. bilioni 75, walikuwa hawajui mfumo wa sasa ni digitali kwamba tumewasajili wakulima tunawajua hadi mtumiaji wa mwisho, TFRA haitalipa hata Sh. 10 hadi tujiridhishe tukikuta mkulima hata mmoja amethirika hiyo imekula kwao (kampuni)," alisema.

"Nimeambiwa Mkurugenzi wa TFRA na meneja wa kanda za nyanda za juu kusini baada ya kugundua wamempiga faini ya Sh. milioni 30, hiyo ni hatua mbaya mimi siijui, ndio shida ya sheria zetu mwizi anapata dirisha la kutokea...nawaambia kwenye kilimo kama umejiandaa kupiga dili imekula kwako," alibainisha.

**RC NJOMBE**

Mtaka aliwataka wafanyabiashara kuwa wazalendo na kuacha ubabaishaji.

"Hii mbolea inahusu wakulima niwaombe Wanajombe wote, watu wa bodaboda, bajaji, makuli wanapoona wanabeba mzigo ambao wanautilia mashaka waendelee kutoa taarifa kwenye vyombo vya serikali kwa sababu hii mifuko 776 ni michanga."

"Hili ghala lipo hapa katikati hakuna tipa la mchanga lilikuja hapa maana yake hii kazi haikufanywa na robot wamefanya binadamu, hebu mtu imuume kuwa anakwenda kuuziwa ndugu yake," alisema.

Mtaka alisema wameshapokea kesi ya mbolea kupunguzwa, kuchanganywa na kuwekwa kwenye mifuko ambayo sio halisi, lakini sasa kumekuja kesi nyingine ambayo mbolea sasa ni mchanga.

Ofisa Masoko wa Kampuni ya Mbolea ya Minjingu, Mshindo Msola, alisema taarifa iko polisi kwa sababu mfanyakazi aliyefanya jambo hilo hayupo.

"Tunashirikiana mtu huyu atafutwe na sisi tuko tayari kushirikiana, tuna imani huyu akipatikana atakuwa ameshatoa suluhu ya jambo hili lililotokea. Sisi kama kampuni limetushangaza, lakini hatukulitegemea," alisema.

Naye Kamanda wa Polisi mkoani Njombe, Hamisi Issah alisema sampuli zimechukuliwa kwa ajili ya hatua za kisheria.


KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA LILILOKO DODOMA

MAOMBI NA. 73 YA MWAKA 2022

SALOME FRUMENCE MASSAWE ....................MDAI 1
JOSEPHINE FRUMENCE MTUI .................... MDAI 2
MADARAKA MACHENYA SAMBAYI.................... MDAI 3

VERSUS

DAUD MICHAEL SAMAMBA .................... MDAIWA

KWA:
DAUD MICHAEL SAMAMBA
POPOTE ULIPO.

YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 28.03. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 27 ya mwezi wa FEBRUARI, 2023.

2173093O2



KUPOTEA KWA VYETI



**MINIA MAKENGO RAMADHANI** natangaza kupotea kwa vyeti vyake Certificate of secondary Education-Kaloleni Islamic Seminary . Certificate of Procurement and Logistic Management. Certificate of Diploma in Procurement and Logistics Management - vilivyotolewa na **TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY** Atakayeviona atoe taarifa polisi :- **ARU/ARU/RB/62614/2023**


# Dola zaadimika Kenya

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI za biashara za Kenya zinakabiliwa na upungufu wa dola za Marekani huku baadhi ya waagizaji bidhaa katika nchi hiyo ya Afrika Mashariki wakikimbilia Tanzania na nchi nyingine jirani kufanikisha biashara zao.

Upungufu huo umekuwa kikwazo kwa watengenezaji na waagizaji wa bidhaa za jumla kutimiza majukumu yao.

Kufuatia uhaba wa dola na ili kulinda akiba, Benki Kuu ya Kenya (CBK) imeamuru benki za biashara kuzuia idadi ya dola zinazotoa.

Wafanyabiashara wengi wa fedha na waagizaji wanadai kuwa benki zimeweka kikomo cha kila siku kwa ununuzi wa dola cha chini ya dola 5,000 kwa sababu biashara zinapata ugumu wa kupata fedha za kigeni za kutosha kukidhi mahitaji yao ya usambazaji.

Kutokana na uhaba huo, wenye viwanda sasa wanalazimika kutafuta dola kutoka kwa wakopeshaji ili kukidhi mahitaji yao.

Benki, hasa taasisi kubwa zaidi, kukosa dola ni changamoto ya kifedha iliyoanza katikati ya mwaka jana nchini humo. "Sasa tunatafuta dola. Nusu tu ya kila benki sita zinaweza kutusaidia kupata dola. Tatu kati ya benki zitatuomba tuangalie baadaye," alisema ofisa mkuu wa kampuni ya utengenezaji bidhaa ambaye hakutaka jina lake litajwe kwa kuhofia kulipizwa kisasi na CBK.

"Kinachopatikana kwenye benki ni kati ya dola 5,000 hadi 10,000. Mtu atakuwa na bahati kupata dola 20,000 na atabahatika sana kupata dola 50,000 kutoka kwa benki moja," alisema.

Waagizaji bidhaa wanadai kuwa wanalazimika kununua dola kwa kiwango cha Sh. 137 za Kenya au zaidi kwa kuwa hawawezi kuzipata kwa kiwango rasmi cha ununuzi cha Sh. 127.39.

Kampuni kubwa zimeanza kufanya biashara ya dola kati yao wenyewe na wale wanaohitaji fedha taslimu wanakimbilia kwenye hoteli na kampuni za ndege.

Hii ni kuvunja sheria na kukuza 'soko la giza' ambalo linaweza kusababisha masuala kadhaa ya kiuchumi, kama vile kuzuia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) na kufifisha soko la FX baina ya benki.

Viongozi wa sekta hiyo wanadai kuwa uwezo wao mdogo wa kupata fedha za kutosha umeathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wao wa kufanya malipo kwa wakati kwa wauzaji bidhaa wa kigeni.

Shirika la wenye viwanda linadai kuwa uhaba wa dola umeathiri uhusiano na wauzaji bidhaa wa nje wakati ambapo ushindani wa kimataifa wa malighafi umeongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji na vikwazo vinavyoendelea vya ugavi.

Upungufu huo unatokana na kuongezeka kwa mauzo ya nje ya malighafi na vifaa kufuatia kuimarika kwa uchumi, jambo ambalo linaongeza mahitaji ya dola.


HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala Iugala, Nala Segu kukamilisha malipo ya viwanja hivyo mapema.

Mwananchi au taasisi itakayoshindwa kulipia kiwanja hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2023 atambue kuwa kiwanja hicho kitauzwa kwa mteja mwingine ili kuboresha huduma katika Halmashauri bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**

Joseph C. Mafuru
**MKURUGENZI WA JIJI**
**DODOMA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S.L.P. 1249,
DODOMA

217303602

HABARI PICHANI

# Wadhamini wa Kampeni ya Mwanamke Kinara 2023 katika uzinduzi



Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) walioshiriki uzinduzi wa kampeni ya MwanamkeKinara2023; kutoka kushoto ni Zainab Ndullah, Gloria Kalinga, Ritha Ngalo na Nancy Massawe.



Meneja Bidhaa wa Kampuni ya Konyagi, Pamela Kikuli, akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya #MwanamkeKinara2023, wao ni moja ya wadhamini wa tukio hilo.



Lilian Malekea kutoka Benki ya NMB na Winfrida Maingu ambaye ni Meneja wa Biashara wa benki hiyo, wakizungumza kwenye uzinduzi wa kampeni hiyo.



Conjester Peter kutoka Idara ya Fedha ya Kampuni ya Bonite Bottlers ambao ni watengenezaji wa maji ya Kilimanjaro, akishiriki uzinduzi huo.

HABARI KITAIFA

# Chongolo kuziweka kikaangoni wizara

**Na Augusta Njoji,** HANANG

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema ataziweka 'kikaangoni' Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Maji ili zimweleze mpango wa kuondoa kero ya barabara na maji kwa baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Hatua hiyo imetokana na malalamiko ya wananchi wa Kata za Bassotu na Hirbadaw waliobainisha kero zinazowakabili ikiwamo ukosefu wa maji na miundombinu ya barabara, hali inayosababisha mazao ya vitunguu na shairi kuoza majumbani kwa kushindwa kuyafikia masoko.

Chongolo, akizungumza na wananchi katika mkutano wa shina namba 16 la wilaya hiyo na alipotembelea Kituo cha Afya Bassotu jana, alisema jukumu la CCM ni kusimamia serikali kuondoa kero zinazowakabili wananchi na atakwenda kukaa na mawaziri husika ili barabara na miradi ya maji ijengwe.

"Eneo hili mnalima sana na ili kusafirisha kufikia masoko, inahitajika miundombinu ya kutosha ya kutoa mazao shambani na kupeleka sokoni, sasa nitakwenda kukaa na Waziri wa Ujenzi aniambie kama Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) imeshapandisha hadhi barabara hii (Singida-Hirbadaw Basodawish hadi Katesh), kujengwa na TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania), kitu gani kinakwamisha ili wananchi waondokane na adha hii?" alihoji.

Alisema barabara hiyo na Haydom-Bassotu hadi Katesh itajengwa kwa lami kutokana na umuhimu wake kiuchumi.

Pia alisema atakwenda kukutana na Waziri wa Maji kujua mpango wa kufikisha maji Bassotu ili kuwaondolea adha wananchi ikiwamo magonjwa ya milipuko.

Vilevile, alitoa mrejesho wa maelekezo aliyoyatoa juzi kwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, kuhusu mpango wa kupeleka dawa na vifaa tiba kwenye hospitali na vituo vya afya vilivyojengwa.

"Juzi Waziri wa Afya alinipigia na nilizungumza naye, akasema wamekaa na MSD (Bohari ya Dawa) kwa ajili ya mpango huo na hadi Juni 2023, vifaa hivyo vitaletwa ili kukamilisha utoaji huduma kwa wananchi kwenye hospitali na vituo vya afya ikiwamo Basout, tunataka majengo mazuri yanayotafsiri na utoaji huduma," alisisitiza.

Kuhusu ujenzi wa madarasa ya kidato cha tano na sita, Chongolo aliitaka serikali kuelekeza nguvu ndani ya miezi mitatu kuanzia mwezi Aprili hadi Julai mwaka huu kujenga madarasa hayo ili kupokea wanafunzi wengi watakaofaulu kidato cha nne.

Alisema kwa sasa shule za serikali zina uwezo wa kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita kwa asilimia 25 hadi 30 na ujenzi huo unapaswa kufanyika ili kufikia asilimia 70.

Kuhusu umeme, alisema hadi kufikia mwezi Juni 2023 vijiji vyote vitakuwa na nishati hiyo na Juni 2024 vitongoji vyote vitakuwa vimefikiwa na huduma hiyo.

Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa CCM, Sophia Mjema, alihimiza viongozi wa mashina kuwa na mikutano ili kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Katibu wa NEC, Idara ya Oganaizesheni, Issa Gavu, alisema CCM ndio yenye uwezo wa kutatua matatizo ya wananchi kutokana na mipango na dhamira iliyonayo.

# THRDC yatoa angalizo kufutwa kwa NGO 4,800

**Na Beatrice Shayo**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) umesema umeshangazwa kufutwa kwa mashirika yasiyo ya kiserikali 4,898 kwa madai ya kukiuka sheria, kanuni na miongozo inayosimamisha shughuli za mashirika hayo.

Aidha, mtandao huo umesema Februari 23, Msajili wa mashirika hayo ametoa notisi kwa mashirika 2,915 kuwa yapo hatarini kufutiwa usajili kwa kushindwa kulipa ada na kuwasilisha taarifa zao kwa zaidi ya miaka miwili.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Wakili wa mtandao huo, Paul Kisabo, alisema idadi hiyo ya mashirika yaliyofutwa ni kubwa haijawahi kutokea katika historia ya nchi.

Kisabo alisema mtandao umeona ni vyema ukufuatilia suala hilo ili kubaini tatizo lilonaloyakumba mashirika hayo na kuendelea kufanya kazi kwa kushirikiana.

Alisema mtandao huo umeguswa na jambo hilo kwa sababu ni shirika huru la wanachama lenye jumla ya mashirika yasiyo ya kiserikali 250 nchini na asilimia 10 ya wanachama wa THRDC ni waathirika wa jambo hilo.

"Tumeguswa na jambo hili kwa sababu mojawapo la jukumu kuu la THRDC ni kufuatilia na kutetea mazingira wezeshi ya watetezi wa haki za binadamu na nafasi za kiraia hapa nchini. Katika kutekeleza jukumu hili THRDC imekuwa ikipitia wakati mgumu, lakini tunashukuru kwa Rais Samia Suluhu Hassan ameweka wazi kuwa watetezi wa haki za binadamu tufanye kazi zetu kwa uhuru na tuzungumze na serikali yake na watendaji wake pale ambapo tumeona mambo hayapo sawa," alisema Wakili Kisabo.

Aidha, Kisabo alisema mtandao umejiridhisha kuwa taratibu zote za kisheria zimezingatiwa katika ufutwaji wa mashirika haya ikiwamo kupewa nafasi za kujitetea.

"Sheria inataka mashirika kuwasilisha taarifa ya mwaka na kulipa ada ya mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 38(2)(b) cha Sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali, kanuni ya 10 pamoja na Jedwali la Pili kwenye Kanuni za mashirika yasiyo ya kiserikali," alisema.

Alisema kama mtandao hawana tatizo na mashirika yaliyofutwa kwa kukiuka sheria endapo kama yalisikilizwa kikamilifu kwa mujibu wa sheria na katiba ya Tanzania na kwamba kutokana na ukubwa wa tatizo la AZISE kutokutimiza masharti ya kisheria huenda yangefutwa mengi zaidi ya hayo.

Wakili Kisabo alisema moja ya sababu ya mashirika hayo kufutwa ni kutokana na mengi yao kutokuwa na fedha za kujiendesha na kusababisha kushindwa kufanya kazi au wakati mwingine mengi kufanya kazi kwa kujitolea.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
TAASISI YA ELIMU TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

**Dar es Salaam, 5, Machi, 2023**

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), inatoa ufafanuzi wa taarifa iliyochapishwa katika Gazeti la Mwananchi la Jumamosi tarehe 4, Machi, 2023 lenye namba ISSN 0856-7573 NA. 8239 yenye kichwa cha habari **Madudu tena Kitabu Kipya cha Hisabati,** kama ifuatavyo:

1. Kichwa cha Habari hii ni upotoshaji kwa kuwa maeneo yaliyotajwa hayaathiri ujifunzaji na ufundishaji na hayapotoshi wanafunzi kama taarifa inavyoeleza. Aidha, taasisi imepokea maoni mbalimbali kutoka kwa watumiaji wa mwisho juu ya ubora wa kitabu tajwa.

2. Sura ya kitabu inayolalamikiwa imeandaliwa kukidhi mahitaji ya muhtasari na ina lengo la kumuwezesha mwanafunzi kupata msingi wa kiuhasibu ili aweze kutumia maarifa haya katika maisha ya kila siku. Kanuni nyingine zote za kiuhasibu zimeelezewa bayana katika vitabu vya masomo ya uhasibu Kidato cha 1-6.

3. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Ofisi ya Kamishna wa Elimu ilitoa Waraka Na. 4 wa Mwaka 2014, kuhusu utayarishaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Katika waraka huo, kazi ya kuandaa vifaa vya kufundishia na kujifunzia inasimamiwa na TET. Ili kufanikisha kazi hii, TET iliandaa miongozo ya uandishi, tathimini na uidhinishwaji wa vitabu vya kiada na ziada. Kwa kutumia miongozo hiyo, uandishi, uhariri na tathimini ya vitabu vya kiada hufanywa kwa kushirikiana na wataalamu bobezi kutoka sekta za umma na binafsi zikiwemo taasisi za elimu za juu, vyuo vya ualimu, na shule. Mpaka sasa TET imeweza kuandika jumla ya vitabu 361 vya kiada na kusimamia uidhinishaji wa vitabu 433 vya ziada, ambapo vitabu vya kiada vinapatikana bure katika maktaba mtandao ya TET kupitia kiunganishi http://ol.tie.go.tz

4. Mwisho, TET inaujulisha umma kuwa imeweka mfumo wa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu machapisho na masuala mengine yote yanayohusu mitaala, vitabu na mafunzo kwa walimu. Maoni hayo ni fursa ya kuendelea kuboresha machapisho hayo na kuhakikisha kuwa yanakidhi mahitaji ya jamii na yanaiwezesha Serikali kufikia azma yake ya kutoa elimu bora kwa kila Mtanzania. Hivyo, wadau wote wanaombwa kutumia fursa hii kutuma maoni kupitia barua pepe ya Mkurugenzi Mkuu kwa anuani ya **director.general@tie.go.tz.**

**Imetolewa na**

**Dkt. Aneth A. Komba Mkurugenzi Mkuu**
**TAASISI YA ELIMU TANZANIA**

217309802

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Simba, Yanga zikizingatia haya robo CAF inazihusu*

**MIAMBA** yenye dhamana ya kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, Simba na Yanga, kesho na keshokutwa, Jumatano itashuka dimbani kucheza mechi zao za nne za hatua ya makundi ya mashindano hayo.

Simba inayoipeperusha bendera ya nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, itakushuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho, Jumanne dhidi ya Vipers ya Uganda wakati Yanga yenye dhamana kama hiyo kwenye Kombe la Shirikisho barani humu, ikiikaribisha Real Bamako ya Mali uwanjani hapo Jumatano.

Hizi ni mechi za marudiano baada ya awali Simba kushinda ugenini bao 1-0, wakati watani zao, Yanga wakilazimisha sare ya bao 1-1 nchini Mali wiki moja iliyopita.

Katika Kundi C, ilipo Simba na pointi zake tatu, inashika nafasi ya tatu nyuma ya vinara Raja Casablaca ya Morocco yenye alama sita na Horoya ya Guinea iliyojikusanyia pointi nne, huku Vipers ikiburuza mkia kwa pointi yake moja.

Kwa upande wa Yanga ambayo ipo Kundi D ikiwa na pointi nne, hadi sasa inashika nafasi ya pili nyuma ya US Monastir ya Tunisia yenye alama saba huku TP Mazembe ya DR Congo ikiwa katika nafasi ya tatu na pointi tatu mbele ya Real Bamako yenye alama mbili mkiani.

Hivyo, katika makundi yote mawili ya wawakillishi hao wa Tanzania, lile la Simba na la Yanga, bado nafasi za kutinga robo fainali zipo wazi kwa kila timu, kinachotakiwa tu ni kila moja kuchanga karata zake vema kwenye mechi mbili mfululizo zijazo za nyumbani kabla ya kwenda kumalizia ugenini.

Kwa mujibu wa ratiba, inaonyesha kuwa rafiki zaidi kwa Simba na Yanga kwani baada ya mechi zao za Jumanne na Jumatano, timu hizo zitashuka tena Uwanja wa Benjamin Mkapa Machi 18 na 19, mwaka huu kuzikaribisha Horoya na US Monastir.

Tunatambua mashabiki hawataziangusha timu zao hususan zinapocheza katika Uwanja wa Mkapa, hivyo kilichobaki ni wachezaji kuelewa hizi si mechi za kucheza 'kirembo' wakimulika kushangiliwa na mashabiki jukwaani, kwani kinachotakiwa ni ushindi wa kishindo kwanza.

Hizi ni mechi za matokeo mbele hivyo kila mchezaji atakayepewa nafasi ya kucheza, anapaswa kutambua lengo ni moja tu, ushindi kwanza na kuweka mbwembwe nyingine kando.


Tunawasihi kutocheza na jukwaa kwani hakutusaidia timu wala mchezaji husika, hasa kwa kutambua ili malengo ya kila upande yatimie hawana budi kusonga mbele kwenye michuano hiyo na hilo si tu litaisaidia klabu, bali hata wachezaji watazidi kupata fursa ya kutangaza vipaji vyao kwa maslahi makubwa zaidi.

Tunaamini kwa idadi kubwa ya mashabiki ambao hujitokeza kutimiza nafasi yao kama mchezaji wa 12 uwanjani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa hususan katika mechi hizi za kimataifa, jukumu kubwa lililobaki ni wachezaji kucheza 'pira mchakamchaka' mwanzo mwisho ili kuwanyima pumzi wapinzani.

Ifahamike ushindi wa Simba kesho na Yanga keshokutwa, ndio utakaoleta morali ya kupambana zaidi katika mechi zijazo kwani utazidi kuzipa nafasi ya kufuzu robo fainali, hivyo ni wakati wa wachezaji kupambana kwa jasho na damu ili kuhakikisha wanapata matokeo katika mechi hizi za Jumanne na Jumatano.

Tunataka kuona Simba na Yanga, msimu huu zikiweka rekodi ya kufuzu hatua ya robo fainali kwa pamoja kwa mara ya kwanza kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika na hilo litawezekana tu kama kila mchezaji, makocha, viongozi na mashabiki watatimiza wajibu wao, hivyo tunawatakiwa wawakilishi wetu hao kila kheri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# *Simba, Yanga, robo fainali kimataifa ipo miguuni mwao*

**KESHO,** Jumanne na Jumatano, Tanzania, hasa jijini Dar es Salaam, kutakuwa na pilikapilika kubwa wakati wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba na Yanga zitakapocheza mechi zao muhimu kabisa.

Simba itacheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers ya Uganda, wakati Yanga Jumatano itakuwa kwenye uwanja huo huo wa Benjamin Mkapa, kumenyana na Real Bamako kwenye Kombe la Shirikisho la Soka barani Afrika.

Kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi kupita, tunashuhudia klabu mbili kubwa zikiwa kwenye michuano hii mikubwa na kila moja ikiwa kwenye nafasi nzuri ya kupata ushindi.

Ukitazama ratiba ya michuano hii ilivyopangwa kwa timu zote mbili, unaona kabisa kuwa kitakachofanya zisisonge mbele kwenye hatua ya robo fainali ni uwezo tu wa uwanjani na wala si kitu kingine chochote.

Ratiba ya michuano hii tangu mwanzo imeonekana si kuzipendelea ila kuzibeba timu za Tanzania. Zote zimeanzia ugenini na kwa bahati mbaya zikafungwa. Simba ikafungwa dhidi ya Horoya ya Guinea bao 1-0 na Yanga mabao 2-0 dhidi ya Monastir ya Tunisia.

Zikarudi nyumbani, Yanga ikashinda 3-1 dhidi ya TP Mazembe, lakini Simba kwa bahati mbaya ilipoteza kwa mabao 3-0 dhidi ya Raja Casablanca.

Halafu zote zikatoka kusafiri tena ugenini, Yanga ikalazimisha sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Real Bamako ya Mali, Simba ikashinda bao 1-0 dhidi ya Vipers ya Uganda.

Ushindi wa Simba ugenini, ukaua mechi iliyopoteza nyumbani dhidi ya Raja Casablanca. Ratiba ikaendelea kuwa rafiki kwa Watanzania kwani zote mbili sasa zinarejea nyumbani kucheza na timu zile zile ambazo zimecheza nazo awali ugenini, tena ikionekana inazimudu.

Ingawa mpira una matokeo matatu, lakini kutokana na mechi za awali ambazo Simba na Yanga zimecheza, kama zikicheza kwa kiwango kile tulichokiona, zina uwezo mkubwa wa kushinda nyumbani.

Mechi za kesho na Jumatano ndizo kwa kiasi kikubwa zitaamua hatma ya timu hizi kimataifa. Pamoja na kwamba zinaweza zisifanye vema, halafu yakatokea matokeo mengine yasiyotarajiwa yakawarudisha kwenye mchezo, ila mechi hizi ndizo zitatoa mwanga halisi na nini zinakwenda kufanya kwenye mechi zijazo.

Kama nilivyosema, ratiba hii iko rafiki, tena kwa timu zote za Tanzania, baada ya mechi hizi, timu hizo bado zitakuwa na mechi zingine hapa hapa nchini. Simba itacheza dhidi ya Horoya Machi 18 na Yanga dhidi ya Monastir Machi 19, mwaka huu. Hapa utaona kuwa robo fainali ya michuano ya kimataifa Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, ipo miguuni mwa wachezaji wenyewe wa timu hizo. Kama watapambana kucheza kufa au kupona na kushinda mechi zote mbili ambazo zitacheza hapa nchini kila moja, basi zinaweza kujikuta zinakwenda kucheza mechi za mwisho zikiwa tayari zimeshatinga robo fainali.

Kwa wachezaji hizi siyo mechi za kucheza 'pira biriani', ni mechi za kucheza bila kuremba, badala yake ni pira la kutafuta nafasi ya kwenda robo fainali ambapo wanapaswa kucheza kwa ari, kupambana na kasi.

Kwa kutumia vitu hivyo vitatu ndivyo vinaweza kukupa matokeo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika na kusonga mbele kwenye mechi hizi zilizopo na si kingine.

Tunaziombea timu zetu ziweze angalau tu kuvuka hatua hii ya makundi ili ziweze kutengeneza pointi ambazo zinaweza kuifanya Tanzania kwa miaka miwili kuweza kupeleka timu nne kwenye michuano ya kimataifa bila tatizo lolote.

Kwa msimu ujao inaonekana ni kama tayari nchi imefanikiwa, kwani kinachotakiwa ni timu yoyote ile kati ya Simba au Yanga imalize nafasi ya tatu kwenye kundi, hapo itakuwa moja kwa moja Tanzania imejiweka sehemu salama bila kujali nchi zingine ambazo nazo zina timu zake hatua ya makundi kwenye michuano hiyo.

Zikivuka hatua hii ina maana tayari zitakiwa zimeshajiwekea akiba ya pointi kwa msimu kwa mwingine baada ya ujao, kwani zitahitaji pointi chache tu ili kufikia malengo.

# Ngumi iliyovunja taya yamponza mahakamani

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imemhukumu Dotto James (26), mkazi wa Mwabasabi wilayani hapa kutumikia kifungo cha mwaka mmoja jela au kulipa faini ya Sh. 100,000 kwa kosa la kumshambulia Augustino Joachim kwa kumpiga ngumi usoni na kumvunja mataya yote mawili na kumsababishia maumivu.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samweli Maweda, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo kuacha shaka yoyote.

Hakimu Maweda alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa vijana wengine wenye tabia za kuwapiga wenzao.

Alisema upande wa mashtaka uliokuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Winfrida Erenesti, uliwasilisha mahakamani mashahidi wanne na kielelezo kimoja cha PF3.

Hakimu Maweda alisema kuwa siku ya tukio, mshtakiwa alimkuta mlalamikaji njiani eneo la Mwabasabi na kuanza kumshambulia kwa kumpiga ngumi usoni na kumvunja mataya yote mawili na kumsababishia maumivu makali.

Hakimu Maweda alisema: "Nimeangalia ushahidi wa pande zote na nimegundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha kosa hili pasipo kuacha shaka yoyote, hivyo mahakama hii inakutia hatiani mshtakiwa kwa kosa ulilošhtakiwa nalo".

Upande wa Mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Winfrida, ulidai mahakamani huko haukuwa na kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa, hivyo ukaomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Hakimu Maweda, kabla ya kutoa hukumu, alisema: "Mahakama hii inakutaka mshtakiwa ujitetee ili upunguziwe adhabu."

Mshtakiwa huyo katika kujitetea, aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana wake wawili na watoto watatu wanaomtegemea.

Hata hivyo, Hakimu Maweda alitupilia mbali utetezi wa mshtakiwa huyo na kusema kitendo ulichokifanya ni kitendo cha kikatili, hivyo mahakama inamhukumu kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 100,000 pamoja na kumlipa fidia mlalamikaji Sh. 300,000 na upande wowote ambao haujaridhika na hukumu hiyo, rufani iko wazi.

Mshtakiwa huyo alilipa faini ya Sh. 100,000 pamoja na fidia kwa mlalamikaji Sh. 300,000, hivyo akaachiwa huru kwenda nyumbani kwake.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Winfrida, alidai mahakamani kuwa Agosti 29 mwaka 2021 huko Mwabasabi, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimshambulia Augustino Joachim kwa kumpiga ngumi usoni na kumvunja mataya yote mawili na kumsababishia maumivu makali, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

## 3,300 waliokatisha masomo wasajiliwa kurejea shuleni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WASICHANA 3,352 wenye umri kati ya miaka 13 na 21 waliokatisha masomo ya sekondari kutokana na sababu mbalimbali, wamejisajili kuendelea na masomo hayo mwaka huu kupitia Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) unaendeshwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW).

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Dk. Michael Ng'umbi, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa Baraza la 13 Wafanyakazi wa TEWW uliofanyika mjini hapa.

Alisema wasichana hao ambao wanaendelea kusajiliwa ni mwendelezo wa mafanikio yaliyopatikana mwaka 2022 ambao walisajiliwa wasichana 3,333 kuendelea na masomo hayo.

Alisema kusajiliwa kwa wasichana hao ambao walikatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo ugonjwa, hali duni ya maisha na kupata ujauzito, kumevuka lengo tarajiwa katika mikakati ya serikali ya kuhakikisha wasichana hao wanapata fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari. Mkurugenzi huyo alisema mradi huo umelenga kuwafikia wasichana wapatoa 12,000 nchini kote kwa kipindi cha miaka mitano ili kuendelea na masomo waliyokatisha kutokana na sababu mbalimbali.

Alisema TEWW imeandaa mitaala na kuendesha programu mbalimbali kwa kutumia mfumo huria na masafa ili kuwafikia walengwa walio wengi zaidi nchini.

Mkurugenzi huyo aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kugharamia ujenzi wa hosteli na kutoa chakula kwa wasichana hao ili kiwe kichocheo cha kuhudhuria masomo hayo ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Akifungua baraza hilo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Michael John aliiagiza TEWW kuhakikisha inasimamia vyema miradi hiyo ili kufikia malengo yote yaliyowekwa.


KUPOTEA KWA VYETI



**TUMAIN RAPHAEL,** Anatangaza kupotelewa na vyeti, Kidato Cha Nne kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sangu Secondary Mwaka 2001 **Index no S0341/0039,** Kidato Cha Sita kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Secondary Sangu Secondary Mwaka 2004 **Index no S0341/0554,** Living Certeficate ya idato Cha nne iliyotolewa na shule ya Sangu Secondary Mwaka 2001, Living Certeficate ya Kidato Cha Sita iliyotolewa na shule ya Secondary Sangu Mwaka 2004 na Living Certeficate of diploma in Education at Mpwapwa. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo Cha Polisi. **TAARIFA YA POLISI: RB NO S1/B.1/2/A/V02.1X/ 182**



TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**TAARIFA KWA UMMA**

**Kusudio la Kufuta Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa Wafanyabiashara Wasio na Sifa za Kuendelea Kusajiliwa katika VAT**

**Dar es Salaam, 01 Machi, 2023:**

Kwa mujibu wa **Kifungu 28** na **29 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148 (Rekebisho la Mwaka 2019),** wafanyabiashara waliotimiza vigezo vya kusajiliwa katika Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), wanatakiwa kuomba usajili huo kwa Kamishna Mkuu. Moja ya vigezo vya kusajiliwa katika VAT ni kuwa na mauzo kwa mwaka, yanayozidi kiwango cha chini kilichowekwa na **Kanuni ya 14 ya Kanuni za VAT za mwaka 2015** cha **Shilingi Milioni Mia Moja.**

Tathmini iliyofanyika kupitia kumbukumbu zetu za usajili wa VAT imebainisha kuwa, baadhi ya walipakodi waliosajiliwa katika VAT, wamepoteza sifa za kuendelea kuwa katika usajili ikiwa ni pamoja na biashara zao kutofikisha mauzo ya milioni mia moja kwa mwaka. Ili kuimarisha usimamizi mzuri katika VAT, Kamishna Mkuu anakusudia kutumia mamlaka aliyokasimiwa chini ya **Kifungu cha 41 cha Sheria ya VAT**, kuwafutia usajili walipakodi wote wenye mauzo chini ya kiwango tajwa, pamoja na wale waliopoteza sifa zilizoainishwa chini ya **Kifungu cha 29 cha Sheria ya VAT. Hata hivyo, kusudio hili halilengi kumuondolea mlipakodi wajibu wake wa kulipa kodi au kuwasilisha ritani za kodi za kipindi cha nyuma kwa walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT.**

Kutokana na ufafanuzi huu, tunawajulisha kuwa **orodha kamili ya majina ya walipakodi wanaotarajiwa kufutiwa usajili wa VAT imewekwa kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz).** Mlipakodi yeyote mwenye pingamizi juu ya maamuzi ya Kamishna Mkuu, anatakiwa kuwasilisha pingamizi lake, akielezea sababu za kwanini asifutiwe usajiliwa VAT. Pingamizi ziwasilishwe katika **Ofisi za TRA kwa Meneja wa Mkoa husika** na **ziwasilishwe ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya notisi hii.** Baada ya siku 30 zilizowekwa kupita, Mamlaka itaendelea na zoezi la kufuta usajili wa VAT.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo

| | |
|---|---|
| **Tovuti:** | www.tra.go.tz |
| **Namba ya Bure:** | 0800 750 075 au 0800 780 078 |
| **WhatsApp:** | 0744 23 33 33 |
| **Barua Pepe:** | huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz |

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

A.J. Kidata
Kamishna Mkuu



Mkurugenzi wa Fedha wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Renata Ndege, akimtwisha ndoo ya maji mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Nyani wilayani Kisarawe, ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa kisima cha maji kilichojengwa na shirika hilo kwenye utekelezaji wa huduma kwa jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jela miaka miwili kula njama kumuua baba yake

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu Matatizo James (40), mkazi wa Kijiji cha Izunya, Wilaya ya Nyanhgwale kutumikia kifungo cha miaka miwili jela kwa kosa la kula njama kumuua baba yake mzazi, James Iboku (72).

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Ntemi Kilekamajenga na aliposomewa mashtaka dhidi yake, alikiri kuhusika kula njama ya kumuua baba yake mzazi kwa madai kuwa walikuwa na mgogoro wa mashamba.

Hukumu hiyo imetolewa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Kilekamajenga, baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa lake.

Upande wa Mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali George Maselo ambaye alidai mahakamani huko kuwa kesi hiyo namba 79/2019 ilikuja mahakamani kwa ajili ya kusikilizwa.

Jaji Kilekamajenga alimuuliza Wakili wa Kujitegemea Forgeth Mongi ambaye alikuwa akimtetea mshtakiwa huyo kama yuko tayari kwa kusikiliza kesi hiyo, naye alidai alikuwa tayari.

Baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa lake hilo, Jaji Kilekamajenga alimwambia Wakili wa Serikali George Maselo amsomee mshtakiwa maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali, Maselo, alidai kuwa katika tarehe tofauti kati Oktoba 2018 na Novemba 2018, mshtakiwa alikula njama ya kumuua baba yake mzazi kutokana na mgogoro wa mashamba.

Wakili huyo alidai mshtakiwa alimkodi Nasoro Hamisi kwenda kumuua baba yake mzazi kwa malipo ya Sh. 500,000 na alimpatia kianzio cha Sh. 120,000 na angetekeleza mauaji hayo, angemalizia malipo yaliyokuwa yamebaki.

Aliendelea kudai mahakamani huko kuwa Novemba 10, 2018, mshtakiwa alimpeleka muuaji huyo nyumbani kwa baba yake ili amtambue na iwe rahisi kutekeleza njama hizo.

Alidai kuwa Novemba 11, 2018, mshtakiwa pamoja na muuaji Nasoro Hamisi walikwenda nyumbani kwa baba yake ili wamuue ndipo baba yake mzazi, Iboku, alipowashtukia na kukimbia kwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Izunya, Wilaya ya Nyaghwale.

Alidai kuwa mwenyekiti alikwenda kutoa taarifa kwenye Kituo cha Polisi Karumwa na mshtakiwa huyo alikamatwa pamoja na mwenzake Nasoro Hamisi na walipofikishwa kituoni, mshtakiwa alikiri kula njama ya kumuua baba yake mzazi kutokana na mgogoro tajwa wa mashamba.

Alidai kuwa baada ya polisi kumaliza upelelezi wa kesi hiyo, mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Baada ya Wakili wa Serikali kumaliza kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali, Jaji Kilekamajenga, alimuuliza mshtakiwa kama maelezo hayo ni ya kweli au la.

Mshtakiwa huyo alidai mahakamani huko kuwa maelezo hayo ni ya kweli tupu.

Baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa lake la kula njama kumuua baba yake mzazi, Jaji Kilekamajenga alisema mahakama inamtia hatiani kwa kosa aliloshtakiwa nalo na kumpa nafasi ya kujitetea ili kupunguziwa adhabu.

Wakili wa Kujitegemea Forgeth Mongi ambaye alikuwa akimtetea mshtakiwa huyo, aliiomba mahakama hiyo impe adhabu ndogo mteja wake kwa kuwa anaishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) na ana familia ya watoto saba na amekaa mahabusu tangu mwaka 2018 alipokamatwa kwa tuhuma za jinai hiyo.

Wakili huyo pia alidai mshtakiwa amejifunza ndiyo maana hakuisumbua mahakama na kuamua kukiri kosa lake, hivyo akaomba mahakama impe mteja wake adhabu ndogo.

Upande wa Mashtaka, ukiongozwa na Wakili wa Serikali Maselo, ulidai mahakamani huko kuwa haukuwa na kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa, hivyo ukaiomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Jaji Kalekamajenga alisema amezingatia hoja tatu kwa upande wa utetezi kwamba ni kweli mshtakiwa huyo amekaa mahabusu kwa muda wa miaka minne; pili mshtakiwa huyo anaishi na VVU na tatu amejutia kosa lake, hivyo mahakama inakuhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha miaka miwili jela.

Jaji Kalekamajenga alisema upande ambao haujaridhika na uamuzi huo, rufani iko wazi.

Akisoma hati ya mashtaka, Karani Msaidizi wa Kumbukumbu wa Mahakama hiyo, Jackline Samweli, alidai mshtakiwa huyo alikula njama ya kumuua baba yake mzazi James Iboku terehe tofauti kati ya mwezi Agosti 2018 na Novemba 11, 2018 kwenye Kijiji cha Izunya, Wilaya ya Nyanghwale, Mkoa wa Geita.

# Kina Mdee kortini tena leo

**Na Grace Gurisha**

KESI ya kupinga kuvuliwa uanachama iliyofunguliwa na wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), inatarajiwa kuendelea kusikilizwa leo baada ya Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam kuiahirisha kwa siku 88 tangu Desemba 6, mwaka jana.

Wabunge hao ni pamoja na Halima Mdee, Grace Tendega, Nursat Hanje, Cecilia Pareso, Hawa Mwaifunga, Esther Matiko, Esther Bulaya, Jesca Kishoa, Felister Njau, Agnesta Lambart, Asia Mohamed.

Wengine ni Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Styella Siyao, Salome Makamba, Anatropia Theonest, Conchesta Lwamlaza na Naghenjwa Kaboyoka.

Kesi hiyo itasikilizwa mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa mahakama hiyo na leo Mbunge Jesca (33) anatarajiwa kuendelea kuhojiwa na jopo la mawakili kuhusiana na kiapo chake alichokiambatanisha kwenye kesi hiyo.

Desemba 6, mwaka jana, mbunge huyo alishindwa kuendelea kuhojiwa na jopo la mawakili wa CHADEMA kutokana na Kiongozi wa Jopo hilo, Peter Kibatala, kutokuwapo mahakamani, mahakama ikiarifiwa kuwa alikuwa kwenye kesi nyingine mkoani Mwanza.

Kutokana na udhuru huo, Jaji Mkeha aliahirisha kesi hiyo hadi leo baada ya pande zote kukubaliana kuiahirisha.

Mdee na wenzake wanawakilishwa na Mawakili Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge na Edson Kilatu huku CHADEMA ikiwakilishwa na Mawikili Kibatala, John Malya, Jeremiah Mtobesya na wengine watatu.

Julai 29 mwaka jana, Wakili Kibatala aliiomba mahakama kuwahoji wabunge wanane kati ya 19 kutokana na viapo vyao walivyoviwasilisha mahakamani huko vikiambatanishwa katika kesi hiyo.

Wakili Kibatala aliwataja wabunge hao kuwa ni Tendega, Hanje, Pareso, Mwaifunga, Matiko, Bulaya, Kishoa na Mdee. Mahakama ilikubaliana na ombi hilo.

Hadi sasa Jopo la Mawakili la CHADEMA tayari limeshamhoji Tendega, Hanje, Pareso na Mwaifunga. Ambao hawajahojiwa kabisa ni Esther Matiko, Esther Bulaya na Halima Mdee.

Wakati wabunge hao wanahojiwa na Wakili Kibatala, walidai kuwa wao ni wanachama halali na wanakipenda chama hicho kwa kuwa walikisotea sana hadi kukaa mahabusu na pia walidai wao sio watu waliokosa akili kiasi cha kujipeleka Dodoma kuapishwa bila kupitishwa na chama chao.

Pia walidai wanashangaa chama hicho kuwakana wao hadharani. Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022, wakiiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza.

Pia wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

Pamoja na mambo mengine, wabunge hao wanadai mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama haukuzingatia matakwa ya kisheria na misingi ya haki, wakidai kuwa hawakupewa haki ya kusikilizwa.

Katika kiapo cha Mdee, anadai kuwa Novemba 25, 2020, CHADEMA ilimtumia barua ya maelezo ya makosa yake kupitia mtandao wa WhatsApp na kumtaka ahudhurie kikao cha Kamati Kuu kilichopangwa kufanyika Novemba 27, 2020, ikiwa na maana kwamba alipaswa kutii wito huo ndani ya siku mbili.



# Madaktari bingwa Hospitali Benjamin Mkapa wapewa 5

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

JOPO la madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Benjamin Mkapa, wamepongezwa kwa utoaji huduma bora kwa wananchi wa Mkoa wa Tanga, tangu walipoweka kambi Februari 27, mwaka huu katika Hospitali ya Rufani ya Bombo.

Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Tanga, Abdalla Rajabu, alitoa pongezi hizo na kusema kwamba huduma hizo ambazo zimetolewa kwa siku tano ni sehemu ya jitihada inayofanywa na serikali kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma za afya.

Alisema chama hicho kitaendelea kuwatia moyo madaktari hao kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kushughulika na magonjwa ya wananchi ambayo pengine yangekuwa chanzo cha jamii kupoteza maisha kwa kukosa matibabu.

"Tuliona ni vyema, sisi kama chama kufika hapa kwa ajili ya kuwapongeza na kuwatia moyo kwa kazi kubwa wanayoifanya, tukifahamu kazi hii ya kuwatibu watu ni kazi ya wito na ndiyo maana hata Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akiongea na madaktari na kuwatia moyo ya kwamba wanachokipata hakilingani na kazi wanazozifanya," alisema Mwenyekiti.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Bombo, Dk. Juma Ramadhan, alisema waliwapokea wataalamu 12, ambao watawasaidia kwenye huduma mbalimbali ikiwamo upasuaji wa mishipa ya fahamu, mifupa, mfumo wa haja ndogo, magonjwa ya ndani, figo, moyo, magonjwa ya watoto, macho, kinywa na meno pamoja na uzazi kwa kinamama.

"Hawa madaktari bingwa wamekuja kutuongezea uzoefu hususani kwa madaktari bingwa ambao tuko nao kwenye hospitali yetu, kiukweli wananchi wa Mkoa wa Tanga wameonyesha mwitikio mkubwa sana wamekuja kupata huduma kwa wingi kila siku, kwa niaba ya Hospitali ya Bombo tunamshukuru Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu kwa kutuletea wataalamu hawa," alisema Juma.

Mtaalamu wa Upasuaji Ubongo na Mishipa ya Fahamu, Dk. Henry Humba, ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, alisema kuwa mpaka sasa wamepokea wagonjwa wengi wenye matatizo ya macho, kwamba takribani watu 194 ambao kati yao 19 wamebainika kuwa na matatizo yanayohitaji upasuaji.

Alisema hadi kufikia sasa, huduma hiyo imewafikia watu zaidi ya 400 tofauti na matarajio ya kuhudumia wagonjwa 200, ambao walitarajiwa kupatiwa huduma ndani ya siku tano.

# BAWACHA yawashukia wanaohujumu Ofisi ya Makamu wa Rais

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

BARAZA la Wanawake la CHADEMA Taifa (BAWACHA), limelaani baadhi ya watendaji wa umma wanaoihujumu Ofisi ya Makamu wa Rais katika mpango wake wa kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Limesema baadhi ya viongozi wa taasisi na halmashauri za Mkoa wa Kilimanjaro zinawazuia kupanda miti katika maeneo yaliyoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Naibu Katibu Mkuu wa BAWACHA, Nuru Ndosi, alitoa tamko hilo juzi wakati wa kampeni ya upandaji miti katika Wilaya ya Hai.

Alisema licha ya kuwapo kwa onyo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, la kuwataka baadhi ya viongozi wanaochangia uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji kuacha ili kunusuru taifa dhidi ya athari za uharibifu zinazojitokeza hivi sasa, lakini bado kuna baadhi ya viongozi hawajamwelewa.

Ndosi alikuwa akiwaongoza wajumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA Taifa, wenyeviti na makatibu wa baraza hilo ngazi ya wilaya na mkoa, kupanda miti katika Shule ya Sekondari Nronga iliyoko Machame Magharibi.

"Huu ni mpango wa kitaifa na hauhusiani na chama. Serikali kupitia kwa Makamu wa Rais (Dk. Mpango), aliagiza upandaji wa miti ufanywe na kila Mtanzania na kuwapo kwa elimu linganifu ya ikolojia, ikiwamo elimu ya uraia ya mazingira.

"Sasa baadhi ya viongozi kwa maslahi yao binafsi, wanachangia uharibifu wa mazingira kwa kuzuia tusipande miti, hii haikubaliki na tunalaani. Waliojaribu kutukwamisha katika kazi hiyo tunaomba wafuatiliwe na wachukuliwe hatua,"alisema.

Juzi, Katibu Mkuu wa BAWACHA, Cathrine Ruge, alieleza jaribio la kuzuiwa kupanda miti hiyo ambalo lilifanywa na Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kiboriloni, Manispaa ya Moshi na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Wakati zuio hilo la upandaji miti katika shule hiyo likitolewa na Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Catherine Ruge, Naibu Katibu Mkuu (Bara), Nuru Ndosi, Wajumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, Suzan Kiwanga na Grace Kiwelu, Mwenyekiti wa CHADEMA, Michael Kilawila, Katibu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema na Lucy Owenya walikuwa wameshafika eneo la tukio hilo.

Baada ya zuio hilo, Ruge alisema baraza hilo liliuchagua Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, ambayo kitaifa inafanyika kuanzia Machi 3 hadi 8 mwaka huu.

"Na katika siku hizo sita tulipanga programu mbalimbali za kuacha alama katika Mkoa wa Kilimanjaro.

"Programu mojawapo ni kupanda miti na tangu asubuhi leo, tumeanzia Zahanati ya Mary Benet (Moshi Vijijini), Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya New St. Anna na baadaye Shule ya Sekondari Kiboriloni. "Lakini kwa masikitiko makubwa tumezuiwa kufanya kazi hii, tumekutana na Makamu Mkuu wa Shule, akasema hana taarifa na ujio wetu na hawezi kuturuhusu kufanya zoezi hili.

"Ingawa tunao viongozi wetu hapa, Diwani wa Kata ya Kiboriloni (Frank Kagoma), alipeleka barua kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi na akasema hakuna shida."

Akieleza namna figisu hizo zinavyoharibu taswira ya umoja wa kitaifa, Katibu Mkuu huyo wa BAWACHA, aliongeza: "Halafu suala la mazingira ni suala la kitaifa, ni suala la maendeleo ya nchi yetu, lakini kwa masikitiko makubwa tumekutana na hiyo changamoto.



Naibu Katibu Mkuu (Bara) Baraza la Wanawake la CHADEMA, Nuru Ndosi (aliyepiga magoti), akipanda mti wa matunda kwenye eneo la Shule ya Sekondari Nronga Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TMDA yachukua hatua uondoshaji bidhaa bandia

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imechukua hatua za kupunguza ongezeko la bidhaa bandia, ambazo zimekuwa zikihatarisha afya ya wananchi. Kaimu Meneja wa Mamlaka hiyo Kanda ya Kaskazini, Dk. Furaha Nyunza, alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, wameamua kutoa elimu kuhusu Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219 ili kuwasukuma kufanya biashara zao kwa kuzingatia sheria na miongozo mbalimbali.


"Lengo la mafunzo haya ni kuwakumbusha wajibu wenu katika kuwahudumia wananchi na kujadili matatizo mbalimbali yaliyopo katika biashara ya dawa vifaa tiba na vitendanishi na kuzitafutia muafaka wake.

"Baada ya mafunzo tunatarajia wadau hawa watafanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa. TMDA ni taasisi iliyoko chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, yenye jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi."

Katika mafunzo hayo, baadhi ya washiriki akiwamo Mkurugenzi wa taasisi ya kutengeneza taulo za kike iitwayo Reepads Sanitary Products, Rephrin Kombe, alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa sababu yatawasaidia kufanya biashara zao kwa kufuata sheria za mamlaka hiyo.

"Kuna watu wamekuwa wakifanya biashara zao bila kufuata taratibu za mamlaka hiyo hali ambayo imekuwa ikihatarisha afya za walaji kwa kutengeneza bidhaa feki, hivyo ni vizuri wakafika katika ofisi za mamlaka hiyo na kuweza kupata taratibu za kufuata,"alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani cha Taasisi ya Usanifu na Uhandisi Mitambo (TEMDO), Elisha Sibale, alisema mafunzo hayo kwao ni muhimu kwa kuwa yanawawezesha kutoa huduma kwa jamii kwa kufuata sheria na taratibu zilizoko.



## Waiomba serikali kudhibiti uvamizi chanzo cha maji

**Na Vitus Audax,** KWIMBA

BAADHI ya wakazi wa Kata ya Ngudu wilayani Kwimba mkoani Mwanza wameiomba serikali kudhibiti vitendo vya uvamizi wa chanzo cha maji Ngudu.

Wamesema chanzo hicho kina uwezo wa kutoa lita 775,000 za maji kwa saa.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti baada ya kushiriki upandaji miti 2,500 katika eneo lililopo chini ya usimamizi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria.

Walieleza kuwa licha ya eneo hilo kutajwa kuwa muhimu kwa taifa bado kuna watu wamekuwa wakivamia eneo hilo na kulishia mifugo pamoja na kuendesha shughuli zao za kilimo.

"Sisi tulipewa elimu tukaelewa thamani ya chanzo hiki ndiyo maana tukaamua kutoka ihali katika eneo hili na kutafuta ardhi nyingine lengo likiwa ni kutunza chanzo hiki, alisema Joseph Njeno-mkazi wa Ngudu.

Mkurugenzi Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria, Renatus Shinho, alisema kutokana na eneo hilo kuwa na uwezo wa kuzalisha kiwango kikubwa cha maji kinaweza kutumiwa na wawekezaji mbalimbali wa viwanda vya maji ya chupa na kuongeza ajira kwa wakazi wa eneo hilo sambamba na kuongeza pato la taifa.

Aliongeza kuwa katika ukanda wa Ziwa Viktoria ni chanzo hicho pekee kilichotambuliwa baada ya uchunguzi wa muda mrefu, hivyo kuna uhitaji mkubwa wa kukitunza sambamba na kutunza miti iliyopo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima pamoja na mambo mengine aliwataka wakazi wa maeneo jirani na chanzo hicho kuacha uvamizi katika chanzo hicho na kuhakikisha wanashiriki katika kutunza eneo hilo ili liwe na faida kwa Taifa.

Balozi wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mrisho Mabanzo, alifurahishwa na shughuli za uhifadhi kupitia upandaji miti.

Hivyo aliiomba serikali kuendelea kuweka mkazo katika kupanda miti pamoja na kuilinda kwa ajili ya kizazi kijacho.

# Hospitali Bugando yaanzisha kliniki kudhibiti msongamano wagonjwa

**Na Vitus Audax,** NYAMAGANA

HOSPITALI ya Rufani Kanda Bugando imekuja na mpango mkakati wa kudhibiti msongamano wa wagonjwa kwa kuanzisha kliniki ya madaktari bingwa.

Kliniki hiyo itakuwa katika eneo la Nera jijini Mwanza, kwamba itakuwa inatoa huduma zote za kibingwa pamoja kuwafikia wananchi wenye uhitaji katika maeneo mbalimbali.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Bugando, Dk. Fabiani Masaga, alibainisha hayo na kuwa hospitali hiyo inapokea wagonjwa wa nje 810 kwa siku sawa na wagonjwa 24,400 kwa mwezi.

Alisema katika kudhibiti hali hiyo wameamua kuja na mpango wa kuanzisha kliniki za nje katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya kanda ya ziwa na magharibi wakianza na Mkoa wa Mwanza.

Alisema mabasi mawili ya kisasa yenye thamani ya Sh. milioni 500 yaliyonunuliwa yatakuwa na kazi ya kuwasafirisha watoa huduma bingwa katika mikoa jirani.

Dk. Masaga alisema kliniki hiyo ya kisasa imegharimu Sh. bilioni mbili ambapo huduma zote zitatolewa kwa mfumo wa kidigitali na siyo kwa mfumo wa karatasi kama ilivyozoeleka. Alisema lengo kuu ni kuondoa ucheleweshwaji wa wagonjwa kupata huduma.

Mwenyekiti wa Bodi ya Hospitali ya Rufani Kanda Bugando,

Askofu Renatus Nkwande, alisema licha ya kuongeza huduma hizo vilevile wameongeza idadi ya wafanyakazi sambamba na madaktari bingwa ambao watarahisisha shughuli za utoaji huduma kwa ufanisi zaidi.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, aliyemwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu katika uzinduzi huo alitoa wito kwa wananchi kutumia fursa ya uanzishwaji wa kliniki hizo kwa kufanya vipimo na kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza




Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, akizindua moja ya mabasi mawili ya kusafirisha madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Rufani Kanda ya Ziwa kuelekea mikoa jirani kutoa huduma kuepusha msongamano wa wagonjwa hospitalini hapo mwishoni mwa wiki. Alimwakilisha Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu katika uzinduzi wa magari hayo pamoja na kliniki ya madaktari bingwa iliyoko Nera jijini Mwanza. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wanafunzi 100 kidato cha kwanza Kishapu hawajaripoti shuleni

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANAFUNZI 101 ambao walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wilayani Kishapu bado hawajaripoti kuanza masomo yao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emmanuel Johnson, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akikagua mahudhurio ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao tayari wamesharipoti katika Shule ya Sekondari Isoso wilayani humo.

Alisema katika wilaya hiyo tangu shule zifunguliwe Januari mwaka huu, jumla ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao tayari wamesharipoti shule ni asilimia 98.17 na kusalia wanafunzi 101 ambao bado hawapo shuleni.

Hivyo aliagiza watendaji wa kata, vijiji na maofisa elimu hadi kufikia Machi 29 wanafunzi hao wote wamesharipoti.

"Mzazi ambaye atazuia mtoto wake wa kidato cha kwanza asiende shule naagiza achukuliwe hatua, hakuna kisingizio chochote sababu elimu ni bure na Kishapu mwanafunzi anaruhusiwa kwenda shuleni hata na sare za shule ya msingi na tukimkuta darasani na sare hizo sisi tuna mnunulia za sekondari,"alisema Johnson.

Aidha, mkurugenzi huyo akiwa katika shule hiyo alikuta wanafunzi wawili wa kike wa kidato cha kwanza wakiwa darasani na sare za msingi na aliwapongeza kwa ujasiri wao kisha akawapatia fedha kwenda kununua sare za sekondari.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Isoso, Annusiatha Buuza, alisema katika shule hiyo wanafunzi ambao walipangwa kujiunga na kidato cha kwanza ni 132, lakini hadi sasa wamesharipoti 130 na kusalia wanafunzi wawili tu.

Nao wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Isoso ambao walikutwa darasani na sare za shule ya msingi akiwamo Kabula Sita, walisema wazazi wao wanakabiliwa na ugumu wa maisha, lakini kutokana na wao kupenda masomo ili bidi wahudhurie shuleni. Walisema walikuwa wanajiona wapweke sababu wanafunzi wote wamevaa sare za shule zinazofanana isipokuwa wao.

# Nipashe Spotika



MBAPPE UKURASA 13




CASEMIRO

# WACHEZAJI 5 WAPYA WALIOBADILI KIWANGO

**LONDON,** England

KUSAJILI wachezaji sahihi ni muhimu kwa mafanikio ya timu za mpira wa miguu. Mafanikio ya timu ya soka yanategemea mambo mbalimbali kama vile kiwango cha ustadi wa wachezaji, kufaa kwao katika nafasi, mtindo wao wa kucheza, utu wao, na uwezo wao wa kufanya kazi pamoja kama timu.

Timu zinapoajiri wachezaji ambao wana wasifu sahihi, wanaweza kuboresha nafasi zao za kufikia malengo yao, iwe ni kushinda taji la ligi au kuepuka kushuka daraja. Zaidi ya hayo, kuwa na wachezaji wanaofaa kunaweza kuongeza ari ya timu na mshikamano, ambayo ni mambo muhimu katika kujenga utamaduni wa timu yenye mafanikio.

Kwa hiyo, kuzingatia kwa uangalifu na kutathmini wasifu wa mchezaji ni muhimu kufanya maamuzi sahihi wakati wa kusajili wachezaji wapya.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano wapya waliosajiliwa ambao wamebadili kabisa hali ya timu.

**#5 Robert Lewandowski (Barcelona)**

Maswali yaliulizwa wakati Barcelona ilipoamua kutoa euro milioni 45 kumsajili Robert Lewandowski msimu uliopita wa majira ya joto. Lewandowski alikuwa anakaribia kutimiza miaka 33 na Barca walipokuwa wakikabiliana na tatizo la kifedha.

Lakini Lewandowski ameleta mafanikio ya muda mfupi. Ameshinda Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya katika misimu miwili iliyopita na ameleta kiwango pale Camp Nou msimu huu. Wakatalunya hao wameteseka kwa misimu miwili iliyopita kutokana na kukosekana kwa mshambuliaji.

Lewandowski amefunga mabao 25 na kutoa pasi za mabao sita katika mechi 31 alizocheza kwenye michuano yote hadi sasa msimu huu. Mabao ya nyota huyo wa Poland na uwezo wake wa uongozi umekuwa na jukumu muhimu kwa Barcelona kukaa kileleni mwa msimamo kwa tofauti ya pointi saba.

**#4 Joao Palhinha (Fulham)**

Fulham imekuwa moja ya timu iliyoonyesha kiwango cha kushangaza kwa msimu huu na mchango wa mchezaji mpya, Joao Palhinha umekuwa msingi wa mafanikio msimu huu. Cottagers hao waliopanda daraja hivi karibuni na wako katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na matarajio yao ya kucheza michuano ya Ulaya msimu ujao.

Fulham ilimsajili Palhinha kutoka Sporting Lisbon kwa kitita cha euro milioni 20 msimu uliopita. Kiungo huyo wa kati wa ulinzi wa Ureno, amekuwa mzuri katikati mwa uwanja kwa kikosi hicho cha Marco Silva.

Ustadi wake wa kushinda mpira haulinganishwi na wachezaji wa Fulham wamefaidika kwa kiasi kikubwa kutokana na kuwa na mchezaji mwamba kama huyo katikati ya uwanja.

**#3 Paulo Dybala (AS Roma)**

Paulo Dybala ni mmoja wa wanasoka mahiri wa kizazi chake. Ingawa kumekuwa na wasiwasi juu ya kiwango chake katika misimu michache iliyopita, alitarajiwa kutowaniwa na timu nyingi wakati alipokuwa mchezaji huru msimu uliopita wa majira ya joto.

AS Roma wakamchukua Dybala na mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina kwa haraka amekuwa muhimu zaidi kwa Giallorossi hao. Katika mechi 23 kwenye michuano yote kwa kikosi cha Jose Mourinho, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amefunga mabao 12 na kutoa asisti saba.

**#2 Casemiro (Manchester United)**

Inajulikana kuwa Erik ten Hag alishinikiza kusainiwa kwa Frenkie de Jong kwa sehemu kubwa ya msimu wake wa kwanza wa kuinoa Manchester United. Lakini hivi karibuni alitambua ukweli kwamba United ilihitaji chuma.

Kwa hiyo, United walielekeza nguvu zao kwa kumsajili gwiji wa Real Madrid, Casemiro. Ilibidi walipe fedha nzuri, euro milioni 70.65 ili kumpata mshindi huyo mara tano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambaye kwa sasa ameiboresha Manchester United.

Ni kwa sifa yake kwamba bado ameweza kupita matarajio na kuwa kipenzi cha mashabiki pale Old Trafford tayari. Casemiro amekuwa na kiwango kikubwa katika safu ya kiungo na ameionyesha Man United kile walichokosa.

Sio tu kwamba amekuwa wa kipekee katika kusoma mchezo na kushinda mpira, lakini ameonyesha uwezo wake bora wa kucheza mpira.

Casemiro pia amefunga mabao muhimu sana kwa 'Mashetani Wekundu' hao msimu huu na alicheza jukumu kubwa katika ushindi wao wa Kombe la Carabao, hata kufunga bao lao la kwanza kwenye fainali dhidi ya Newcastle United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amefunga mabao matano na kutoa pasi za mabao sita katika mechi 35 alizocheza kwenye mashindano yote kwa upande wa kikosi hicho cha kocha Ten Hag hadi sasa msimu huu.

**#1 Khvicha Kvaratskhelia (Napoli)**


Napoli ilimsajili Khvicha Kvaratskhelia kutoka Dinamo Batumi kwa euro milioni 11.5. Kinda huyo anachukuliwa kuwa mchezaji bora wa msimu wa 2022-23 barani Ulaya. Kvaratskhelia amemfurahisha kila mtu kwa uwezo wake.

Tayari amekuwa kipenzi cha mashabiki pale Napoli na amepata jina la utani 'Kvaradona'. Vitendo vya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, vimesaidia sana kuifanya Napoli kuwa timu yenye nguvu zaidi nchini Italia kwa tofauti kubwa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Georgia, amefunga mabao 12 na kutoa pasi nyingi za mabao 15 katika mechi 26 pekee kwenye mashindano yote akiwa na 'Partenopei' hao hadi sasa msimu huu.

## ISIKUPITE

Cristiano Ronaldo ameiwezesha miamba ya Ligi Kuu Saudi Arabia, Al-Nassr kufikisha wafuasi milioni 150 kwenye mtandao wa kijamii wa Instagram kwa Januari mwaka huu. Idadi hiyo inaifanya Al-Nassr kuzipiku klabu kubwa za Ulaya zikiwamo Man Utd, Man City, Chelsea, Arsenal, Bayern Munich na Liverpool. Hivyo kushika nafasi ya nne kwenye klabu za soka zenye wafuasi wengi ikiwa nyuma ya vinara Barcelona (milioni 203), Paris Saint-Germain (milioni 207) na Real Madrid (milioni 209).



# KWA NINI EPL LIGI BORA DUNIANI?


Moja ya mechi za kusisimua Ligi Kuu England katika Uwanja wa Emirates juzi. Hapa wachezaji wa Arsenal na benchi lao la ufundi wakishangilia baada ya juzi kushinda mabao 3-2 wakitokea nyuma dhidi ya Afc Bournemouth.

**LONDON, England**

LIGI Kuu England, EPL, ni ligi ya daraja la juu ya soka la kulipwa nchini humo. Ilianzishwa mwaka 1992, baada ya uamuzi wa Klabu za Ligi ya Soka za Daraja la Kwanza kujiondoa kwenye daraja hilo, ambapo ilikuwapo tangu mwaka 1888.

Kujitenga kulilenga kuongeza uwezo wa kibiashara wa ligi na kujadili mikataba bora ya utangazaji na udhamini. Msimu wa kwanza wa EPL ulianza Agosti 15, 1992 na Manchester United wakaibuka mabingwa wa kwanza.

Tangu kuanzishwa kwake, EPL imekuwa miongoni mwa ligi za soka maarufu na yenye fedha nyingi zaidi. Mafanikio ya ligi hiyo yanaweza kuchangiwa na mambo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ubora wa soka unaoonyeshwa, malipo ya fedha yanayotolewa na mvuto wa kimataifa wa wachezaji nyota.

Pia inasifika kwa ushindani wake, huku timu kadhaa zikishinda taji hilo kwa miaka mingi. Manchester United imekuwa timu yenye mafanikio zaidi katika zama za EPL, ikiwa na mataji 13, ikifuatiwa kwa karibu na Manchester City yenye mataji sita na Chelsea yenye mataji matano.

Katika miaka ya hivi karibuni, ligi hiyo imeendelea kupanua wigo wake, huku mashabiki wengi zaidi wakifuatilia kutoka duniani kote. Umaarufu wake duniani umechochewa kwa sehemu na kuongezeka kwa mitandao ya kijamii ambayo yamerahisisha zaidi kuliko hapo awali kwa mashabiki kufuatilia timu na wachezaji wanaopenda.

Juhudi kubwa zimefanywa ili kukuza ligi hiyo sehemu nyinginezo, huku ziara za kabla ya msimu mpya na matukio ya utangazaji zikifanyika katika nchi kama vile China, Marekani na Australia. Leo, EPL inachukuliwa kote duniani kuwa mojawapo ya ligi ya soka inayosisimua na yenye hadhi kubwa zaidi na yenye mashabiki waaminifu kutoka mabara yote.

Kwa kuzingatia hilo, hebu tuangalie mambo sita yaliyochangia EPL kuwa ligi bora zaidi ya soka duniani.

**1. Ufikiaji wa kimataifa**

Kuonekana kwa Ligi Kuu duniani kote kumechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha hadhi yake kama ligi bora zaidi duniani. Moja ya faida kuu za mvuto wa ligi duniani kote ni ongezeko la mapato inayozalisha. Ikiwa na hadhira ya kimataifa ya zaidi ya watazamaji bilioni tatu, ndiyo ligi ya soka inayotazamwa zaidi duniani. Hii imevutia wafadhili na watangazaji wa kimataifa na kusababisha malipo makubwa ya kifedha kwa klabu na wachezaji.

EPL imevutia baadhi ya wachezaji bora zaidi duniani na kuongeza zaidi ufikiaji wake kote duniani. Mbali na faida za kifedha, kuonyeshwa kwa ligi hiyo duniani kote pia kumesaidia kuinua hadhi ya soka la Uingereza na klabu zake. Huku mashabiki kutoka kila pembe ya dunia wakifuatilia ligi hiyo na kujifunza historia na utamaduni wake.

Hii imesababisha kuthaminiwa kwa historia na mila za timu na kuongezeka hamu ya watu wengi kuitembelea England kutazama mechi moja kwa moja.

**2. Dabi za kusisimua**

Mechi za Dabi (klabu za mji mmoja), ni sehemu muhimu ya ligi yoyote ya soka na zimechangia kwa kiasi kikubwa kuinua hadhi ya kuwa Ligi Kuu bora zaidi duniani. Mechi hizi huhusisha timu kutoka jiji au eneo moja na zinajulikana kwa ushindani wao mkubwa na mashabiki wenye mizuka. Mechi za dabi mara nyingi huwa na ushindani wa hali ya juu, huku wachezaji wakijitolea kila kitu ili kupata ushindi kwa timu yao.

Moja kati ya mechi zenye hadhi ya juu ni dabi ya Manchester inayoshirikisha timu mbili kubwa - Manchester United na Manchester City. Upinzani kati ya timu hizo mbili ulianza kwa zaidi ya karne moja na umezalisha matukio ya kukumbukwa katika historia ya Ligi Kuu. Mechi zingine zinazojulikana ni pamoja na Dabi ya London Kaskazini kati ya Arsenal na Tottenham Hotspur, Merseyside Dabi kati ya Liverpool na Everton na Tyne-Wear Dabi kati ya Newcastle United na Sunderland.

**3. Kutotabirika**

Ligi Kuu England inasifika kwa staili ya uchezaji wa nguvu na matokeo yasiyotabirika, huku baadhi ya mechi za soka za kusisimua zaidi duniani zikifanyika kwenye viwanja vyake. Mtindo wa uchezaji wa ligi unaoshika kasi na unaotumia nguvu nyingi ni sababu kuu katika mvuto wake wa kimataifa, huku mashabiki duniani kote wakifuatilia kutazama baadhi ya wachezaji bora wakishindana.

Ligi hiyo imeshuhudiwa matukio ya kukumbukwa katika soka, ikiwa ni pamoja na kumaliza kwa kasi kwa mbio za ubingwa na kushuka daraja ambapo timu zimenusurika katika nafasi zinazoonekana kutowezekana.

Mfano mmoja kama huo ni msimu wa 2011/12, ambao ulishuhudia Manchester City ikishinda taji kwa mtindo wa ajabu katika siku ya mwisho ya msimu. City walifunga mabao mawili katika dakika za majeruhi na kupata ushindi na kubeba taji.

Msimu mwingine wa kukumbukwa ulikuwa wa 2015/16, ambao ulishuhudiwa Leicester City wakishinda taji hilo kinyume cha matarajio.

Mifano hii inaonyesha mvuto wa kipekee wa Ligi Kuu na hatua ya kusisimua ambayo imeifanya kuwa ligi bora zaidi duniani.

**4. Mashabiki vichaa**

Mashabiki wa kusisimua ('vichaa') wamekuwa jukumu muhimu katika kuifanya ligi hiyo kuwa bora zaidi duniani. Mashabiki hawa wanajulikana kwa sapoti yao isiyoyumba, bila kujali uchezaji wa timu yao. Wanaunda hali ya kipekee katika viwanja ambavyo. Nguvu na shauku ya mashabiki kwenye mechi hutoa mchango mkubwa kwa uchezaji wa wachezaji, hivyo kuwatia moyo kufanya vema wawezavyo.

Mifano mashuhuri ya mashabiki vichaa ni pamoja na wale wa Liverpool, maarufu kwa kuimba kwao kwa mapenzi ya "You'll Never Walk Alone." Wimbo huu umekuwa sawa na klabu na huimbwa katika kila mchezo wa nyumbani. Mfano mwingine mashuhuri ni mashabiki wa Manchester United, ambao wanajulikana kwa wimbo wao maarufu, "Glory, Glory Man United," ambao umekuwa moja ya nyimbo zinazotambulika zaidi duniani.

Ligi Kuu England pia ni kati ya ligi zilizohudhuriwa na mashabiki wengi zaidi duniani. Kwa mujibu wa mtandao wa statista.com, EPL iliandikisha idadi kubwa zaidi ya mahudhurio katika ligi tano bora za Ulaya msimu wa 2021/22 - ikiwa na wastani wa watazamaji 39,632 kwa kila mchezo. Hii inaangazia zaidi kujitolea kwa mashabiki kwa klabu zao.

**5. Ushindani mkali**

EPL inajulikana kwa ushindani wake mkali, huku baadhi ya timu bora za soka na wachezaji duniani wakichuana. Hali ya ushindani ya ligi imekuwa na jukumu muhimu katika maendeleo yake ya kuwa moja ya ligi bora zaidi duniani. Presha ya mara kwa mara ya kufanya kiwango cha juu zaidi imezifanya timu kuinua mchezo wao na kusababisha kiwango cha juu cha soka. Hii imeunda utamaduni wa ubora, ambapo wachezaji na timu hujisukuma kila mara kuwa bora.

Mifano maarufu ya ushindani mkali wa ligi hiyo ni pamoja na ushindani mkali kati ya Manchester United na Arsenal kati ya mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000. Timu hizo mbili zilitawala soka la England.

Mfano mwingine ni mchuano wa hivi karibuni kati ya Manchester City na Liverpool, huku timu hizo zikisukumana hadi kikomo katika mbio za kusisimua za ubingwa katika misimu ya 2018/19 na 2021/22. Mifano hii inadhihirisha jinsi ushindani mkali wa Ligi Kuu ulivyopelekea ligi hiyo kuimarika na kuwa bora zaidi duniani.

**6. Wachezaji, makocha wa kiwango cha kimataifa**

Kununuliwa kwa wachezaji na makocha wa kiwango cha kimataifa na Klabu za Ligi Kuu kumekuwa sababu kubwa ya kuifanya ligi hiyo kuwa bora zaidi duniani.

Ligi hiyo inavutia baadhi ya majina yanayotafutwa sana katika mchezo huo, hivyo kusababisha kiwango cha juu cha soka. Ligi hiyo imekuwa kivutio cha wachezaji na makocha wakuu kutokana na hali yake ya ushindani, mishahara mikubwa na kudhihirishwa kimataifa. Ujio wao umeleta viwango vipya vya msisimko na ustadi kwenye ligi na kuifanya kuwa ya kufurahisha na kusisimua zaidi kwa mashabiki.

Makocha kama Sir Alex Ferguson, Arsene Wenger, Pep Guardiola, Jose Mourinho, Jurgen Klopp, Carlo Ancelotti na Antonio Conte ni miongoni mwa waliotamba zaidi kwenye mchezo huo na wamesaidia kuinua hadhi ya ligi hiyo kuwa moja ya ligi bora zaidi duniani. Kuajiriwa kwa kocha kama Unai Emery, ambaye aliiongoza Villarreal kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021/22, na Aston Villa iliyo hatarini kushuka daraja kunazungumza mengi.

Vile vile, EPL haijawahi kukosa wachezaji wa kiwango cha kimataifa. Kando na mastaa wakubwa wa nyumbani, Klabu za England havijawahi kuona aibu kutumia fedha ili kunyakua vipaji kutoka nje ya nchi. Thierry Henry, mfungaji bora wa muda wote wa Arsenal, aliwasili kutoka Monaco mwaka 1999 na kuwa mchezaji wa kigeni bora zaidi kuwahi kutokea kwenye ligi hiyo. EPL pia inazidi kuwa mahali pa kupendelewa zaidi kwa nyota wanaochipukia kote duniani, huku Erling Haaland akipendelea kuhamia Manchester City badala ya timu zingine zenye nguvu za Ulaya kumwania.

## Nukuu

"[Erling Haaland] anahitaji timu kufunga mabao. Yeye si kama Messi [Lionel], kama vile anaweza kwenda kuchukua mpira, kupiga chenga na kukokota mpira kwa kuwapita [wachezaji] watatu au wanne. Anaweza kuamua mchezo mwenyewe. Erling anahitaji timu. Sio yote juu yake. Lazima tutafute, lazima nitafute njia, kwa wachezaji, katika hali ya aina hii," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akielezea tofauti kati ya Messi na Haaland**



"Kutwaa Kombe la Dunia lilikuwa jambo bora zaidi lililotokea katika kazi yangu, namshukuru Mungu ambaye alinisaidia kufanikiwa baada ya miaka mingi ya kujaribu," **Mshambulizi wa Paris Saint-Germain na Argentina, Lionel Messi, akieleza kwa furaha baada ya kushinda tuzo yake ya saba ya FIFA ya Mchezaji Bora wa Kiume wa Mwaka.**



"Nilijua nitavunja rekodi hii. Kucheza hapa ni fursa. Nilikuja hapa kama mchezaji kinda. Nimejifunza mengi hapa, kama mwanaume pia. Kucheza PSG, hata zaidi kwangu kama mzaliwa wa Paris, ni maalum. Siku zote nilisema kwamba nilitaka kuandika historia Ufaransa, katika mji mkuu, katika nchi yangu, katika jiji langu. Ninayoifanya ni nzuri, lakini bado kuna safari ndefu ya kwenda. Ni mafanikio ya kibinafsi, lakini nilikuja kwa mafanikio ya pamoja," **Mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe, baada ya juzi kuvunja rekodi ya Edinson Cavani ya mabao 200 na kuwa mfungaji bora wa wakati wote wa klabu hiyo wakati wakishinda 4-2 dhidi ya Nantes juzi.**





Straika wa Azam FC, Prince Dube, akijaribu kumlamba chenga beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara Februari 21, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1. Kwenye mechi hiyo, Dube aliweka rekodi ya kufunga bao linaloshikilia rekodi la kuwa la mapema zaidi mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, sekunde ya 15 ya mchezo.

# MABAO YA 'ASUBUHI' ZAIDI LIGI KUU TANZANIA BARA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara inasimama wiki hii kupisha mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho Afrika na michuano ya Kombe la FA la Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), ikiwa kwenye raundi ya 24.

Zimesalia raundi sita tu ili kumaliza Ligi Kuu msimu wa 2022/23, ambapo bingwa atajulikana pamoja na timu zingine mbili ambazo zitapata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Mashabiki pia watafahamu timu mbili zitakazoshuka na idadi kama hiyo zitakazokwenda kucheza mechi za mchujo na timu za Championship ambazo zitashika nafasi ya tatu na nne.

Mpaka sasa tumeona rekodi na takwimu nyingi zikiwekwa na timu zote zinazoshiriki, ziwe nzuri au mbaya kwa upande wao.

Wachezaji pia wamekuwa wakishindana kuweka, au kutengeneza rekodi mbalimbali za kuvutia. Hata hivyo, wapo wachezaji ambao wana rekodi zisizo za kuvutia kama kuwa na kadi nyingi za njano, nyekundu, kujifunga wenyewe na vingine vinavyofanana na hivyo.

Leo tutaangalia rekodi za wachezaji waliofunga mabao ya mapema zaidi kwenye Ligi Kuu hii inayoendelea...

**Prince Dube - Azam (sekunde ya 15)**

Straika huyu raia wa Zimbabwe ndiye mchezaji anayeshikilia rekodi tamu ya kufunga bao la mapema zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Alifunga bao sekunde ya 15 tu kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo na Simba, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Februari 21, mwaka huu, mchezo ukimalizika kwa sare ya 1-1, Simba ikirudisha bao hilo muda mfupi tu kabla ya mechi kumalizika, likiwa ni la kujifunga la Abdallah Kheri 'Sebo.'

Simba ndiyo waliuanza mpira, kwa kuurudisha nyuma, halafu ukapigwa kwenye wingi ya kulia ambako beki wa kushoto Mohamed Hussein 'Tshabalala' alikuwa amepanda kuufuata kabla hajaupata, beki wa kulia wa Azam FC, Nadhan Chilambo aliupiga kichwa, ukaenda kwa Daniel Amoah aliyetoa pasi fupi kwa James Akaminko, akageuka na kummegea pande refu lililonyooka kama rula kwa Dube.

Ilipigwa kwenye njia, katikati ya beki wa kati wa Simba, Kennedy Juma na Henock Inonga. Aliwapita kama kipanga, akauwahi mpira na kuujaza wavuni, kipa Aishi Manula akiwa ametoka golini kutaka kuuwahi mpira. Matukio yote haya, yalitokea muda mfupi yakitumia sekunde 15 tu.

**Nickson Kibabage - Mtibwa (sekunde ya 58)**

Anayefuatia ni Nicksona Kibabage wa Mtibwa Sugar, ambaye alifunga bao lake sekunde ya 58 kwenye mechi dhidi ya Mbeya City Oktoba 2, mwaka jana kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Kipa wa Mbeya City Haroun Mandanda aliupiga mpira mbele, ukanaswa na James Kotei, akaupeleka kwa George Chota, akammegea pande Kibabage ambaye aliukwamisha wavuni.

Mechi hiyo iliisha kwa timu zote kufungana mabao 2-2, Jean Pipi Matore akiifungia Mtibwa na mabao ya Mbeya City yakifungwa na Tariq Seif pamoja na Faruk Shikhalo aliyejifunga.

**Ismail Mgunda - Prisons (dakika ya kwanza)**

Aron Kalambo wa Dodoma Jiji alimchezea madhambi Hamisi Mcha na kusababisha mkwaju wa penalti. Ikakwamishwa nyavuni na Ismail Mgunda dakika ya kwanza ya mchezo, akiingia kwenye kitabu cha wachezaji waliofunga mabao ya mapema zaidi kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Tuta hilo lilipatikana kwa Ibrahim Abraham kupiga ndefu baada ya mechi kuanza na hauonekana kuwa na madhara, lakini beki Amani Kyata aliporuka juu kumrudishia kipa wake, haukwenda kwa kasi inayotakiwa, huku Mcha akiwa anakuja mbio, kuudokoa, lakini wakati huo huo akakatwa kiatu na kipa wa Dodoma Jiji.

Mechi hiyo ilichezwa Agosti 21, mwaka jana Uwanja wa Liti, Singida, na kumalizika kwa Prisons kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. Jeremiah Juma aliifungia Prisons bao la pili kabla ya Hassan Mwaterema kufunga goli pekee la Dodoma Jiji.

Moses Phiri - Simba (dakika ya pili)

Aliuchukua mpira uliokosewa na Baraka Majogolo, akaukokota kwa umbali, mrefu kabla ya kuwageuzageuza mabeki wa KMC kama chapati, mwishowe aliachia shuti la mguu wa kushoto lililotinga ndani ya wavu.

Ilikuwa ni dakika ya pili ya mchezo huo, bao hilo likifungwa na straika wa Simba raia wa Zambia, Moses Phiri, Septemba 7, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya KMC, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2.

Habib Kyombo aliipatia Simba bao la kusawazisha dakika za mwisho za mchezo, mabao ya KMC yakiwekwa kimiani na Matheo Antony na George Makang'a.

**Ali Kipemba - Polisi Tanzania (dakika ya tatu)**

Nafasi ya tano imechukuliwa na straika wa Polisi Tanzania, Ali Kipemba ambaye alifunga bao dakika ya tatu ya mchezo, Agosti 21, mwaka jana, Uwanja wa Shekh Amri Abeid, Arusha, timu yake ikicheza dhidi ya KMC na mechi kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Alikuwa ni Salum Chukwu aliyeambaa na mpira kwenye wingi ya kulia na kuingia nao ndani, kabla ya kupiga shuti lililopanguliwa na kipa Nurdin Balora, ukamkuta mfungaji akaukwamisha wavuni.

Chilo Mkama aliifungia bao la pili, huku KMC wakifunga mabao yote mawili kupitia kwa Matheo Anthony.

**Matheo Antony - KMC (dakika ya tatu)**

Aliruka juu na kuunganisha krosi iliyopigwa kulia mwa uwanja, mpira ukajaa wavuni, ukimuacha James Ssetuba wa Ihefu akiwa hana la kufanya.

Huyo ni straika wa KMC, Matheo Antony, akifanya hivyo Septemba 20, mwaka jana kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salam, naye akiwa kwenye nafasi ya tano kama Ali Kipemba, wote wakifunga kwenye dakika ya tatu ya mchezo.

Ni mechi ambayo KMC iliondoka na ushindi wa mabao 2-1, Nzigamasabo Steve akifunga bao la pili, Rarael Daudi akitupia la kufutia machozi kwa Ihefu.

**JE, WAJUA?**




Kylian Mbappe kwa sasa ndiye mfungaji bora wa wakati wote wa Paris Saint-Germain (PSG) akiwa na mabao 201 baada ya juzi kuvunja rekodi iliyokuwa ikishikiliwa na Edinson Cavani ya mabao 200. Mbappe, 24, ametimiza na kupita rekodi hiyo akiwa na mechi chache alizoichezea klabu hiyo (247), wakati mshambuliaji huyo wa Kimataifa wa Uruguay yeye alitimiza mabao 200 baada ya mechi 301.



## HABARI DODOMA

## Wahitimu sekondari watakiwa kukemea vitendo ulawiti, ubakaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wanafunzi wanaojiandaa na mitihani ya kuhitimu kidato cha sita kutojihusisha na vitendo vya ulawiti na ubakaji.

Badala yake amewataka waendeleze tabia ya uadilifu waliyokuwa nayo wakati wakiwa shule.

Alitoa ushauri huo wakati wa mahafali ya kuwaaga wanafunzi 460 wa kidato cha sita ambao ni wanachama wa klabu za wapinga rushwa kutoka shule mbalimbali za sekondari zilizoko mkoani hapo.

Pamoja na mambo mengine aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kulifanyia kazi suala la uanachama wa kudumu kwa wanafunzi wanaohitimu, ili kuhakikisha wanakuwa mabalozi wazuri wa rushwa, ikiwamo kutambulika hata kama watakuwa wamemaliza masomo yao.

Alisema elimu walioipata shuleni kuhusu nidhamu na uadilifu kwenye suala zima la rushwa wanapaswa kuiendeleza wakiwa uraiani, hususani utoaji elimu kwa raia ambao hawana uelewa na madhara ya rushwa.

"Wanafunzi msiende kujiunga na mambo yasiofaa, kaendelezeni mazuri mliofundishwa katika suala zima la kupinga rushwa katika maeneo mbalimbali mnayotoka,"alisema Senyamule.

Alisema wanategemea kuwaona wanafunzi hao wanakuwa mabalozi wazuri katika maeneo wanayotoka, ikiwamo kuwa chachu ya utoaji elimu katika suala zima la kupiga vita rushwa ambayo haikubaliki.

Senyamule alifafanua kuwa hivi sasa taifa linapambana kuzuia vitendo vya rushwa, hivyo nao wanapaswa kuonyesha jitihada hizo wakiwa uraiani na kuongeza kuwa wakifanya hivyo taifa litakuwa na viongozi waadilifu.

Akizungumzia kuhusu suala la uanachama kwa wanafunzi wanaohitimu, alisema TAKUKURU inapaswa kulifanyia kazi ili wahitimu hao waweze kutambulika na kuendelea kutoa elimu ya kupiga vita rushwa kwa jamii. Mbali na hilo amezipongeza klabu za wapinga rushwa ambazo ziko hai, huku akisisitiza kuendelea kuzisimamia kwa sababu zinawajenga vijana wakiwa awali kukataa vitendo vya rushwa ambayo inachangia kupata viongozi wazembe.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema jukumu la kupiga vita rushwa ni la kila mmoja, hivyo wanafunzi wanaohitimu wanapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwenye mapambano hayo.

Alisema wanaendelea kuzihamasisha shule zote mkoani Dodoma kuwa na klabu za kupinga rushwa huku akisisitiza vijana hao waliohitimu wameiva vizuri, hivyo wanakwenda kuwa mabalozi wazuri.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimwer, aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii ili waweze kufanya vizuri mitihani yao ya kidato cha sita.

Mbali na hilo alisema katika shindano la mdahalo kuhusu kupiga vita rushwa baina ya shule na shule amepanga kutoa zawadi kwa washindi.

# Ukosefu elimu afya ya uzazi chanzo umaskini katika jamii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUKOSEKANA kwa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana walio katika lika la balehe kumetajwa kuwa chanzo cha umaskini kwa kundi hilo na jamii.

Hayo yalielezwa juzi na Ofisa wa Shirika la Action Aid, Rahim Nasser, wakati wa kikao kilichowakutanisha vijana wa lika balehe kutoka Wilaya ya Mbozi na Kilosa.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kujadili umaskini, visababishi vya umaskini mifumo, mila, desturi na sera ambazo zimekuwa zikimkandamiza mwanamke kuwa nyuma katika kupata elimu.

Rahim alisema inafahamika kwamba elimu ndiyo ufunguo wa maisha kwa sababu inampa kijana uwezo wa maisha yake ili kuweza kuyatumia kikamilifu.

"Kama katika jamii kuna kundi halitapata elimu hivyo basi kundi hilo linaandaliwa kuwa maskini ambapo kundi hilo halitakuwa na uwezo wa kushughulika na mazingira yake," alisema.

Aliongeza: "Hali halisi ya jamii zetu na mifumo na tamaduni zetu zimemfanya mwanamke asipate elimu kama mwanaume wakati wanawake ni kundi kubwa na takwimu zinaonyesha wanawake ni wengi kuliko wanaume, hivyo kama kundi hili halitapata elimu moja kwa moja uchumi wa nchi unapungua kwa asilimia 50".

Alisema afya ya uzazi ni kitu mojawapo kati ya vitu vingi ambavyo huenda vikasababisha wanawake au vijana balehe kuwa maskini ndani ya jamii zao.Alisema kutokana na hali hiyo, Action Aid imejipanga kuboresha huduma ya afya ya uzazi kwa wanawake na wanaume kwa kupewa elimu sawa ili kuondoa hali ya mwanamke kupewa vipaumbele kwa nafasi maalum na badala yake wapewe uwezo wa kuweza kupambana na kujisimamia wenyewe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la ICAO linalojihusisha na masuala ya vijana, Zahara Salehe, alisema wanafanya kazi kwenye maeneo yanayowahusu vijana.

Alisema hapa nchini imeonekana vijana wana mambo mengi yanayowahusu na yanayotakiwa kufanyiwa kazi hususani eneo la afya ya uzazi ambapo takwimu zinaonyesha maambukizi kwa vijana yanaongezeka na mimba za utotoni kwa wanafunzi wa shule ya msingi.

Akizungumza kwa niaba ya vijana wenzake, Rhoida Samson kutokea Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro alisema amepata mafunzo ya afya ya uzazi na ataitumia elimu hiyo kuelimisha wenzake.



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Ramadhani Kailima, akizungumza na watumishi wa tume hiyo ikiwa ni mara ya kwanza tangu alipoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Malalamiko uchafuzi mazingira, muziki yapokelewa NEMC

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limesema katika kipindi cha miezi nane limepokea na kushughulikia malalamiko 369 yaliyohusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira ikiwamo kelele za muziki kwa wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Samwel Gwamaka, aliyasema hayo jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za NEMC.

Alisema malalamiko hayo yamepokelewa katika kipindi cha Julai 2021 hadi Februari 2022 ambayo ni kuvuja kwa mafuta kutoka kwenye mabomba ya mafuta, kuchoma taka hatarishi chini ya kiwango kinachotakiwa kisheria, uchafuzi wa vyanzo vya maji, utiririshaji wa majitaka, uchafunzi wa hewa kutokana na shughuli za viwanda.

Mengine ni kelele za muziki, kushamiri kwa gereji bubu maeneo ya makazi, kushamiri kwa vituo vya mafuta katikati ya makazi, matumizi ya mifuko ya plastiki kutapakaa maeneo ya makazi.

Aidha, alisema kwa kipindi hicho NEMC imekuwa ikishughulika na udhibiti wa taka ngumu kama vile utekelezaji na utoaji wa vibali ambapo uteketezaji wa taka hatarishi kama dawa na bidhaa za viwandani zilizokwisha muda wake umefanyika.

Dk. Gwamaka alisema kwa kipindi hicho NEMC imeanzisha kanda tisa nchini zenye wataalamu wa mazingira wanaotekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 wakishirikiana na wadau, halmashauri za miji na wilaya hali iliyorahisisha utatuzi wa kero za kimazingira.

Kuhusu tathmini ya athari kwa Mazingira (TAM) kwa kipindi hicho, alisema NEMC imesajili miradi 1,702, ambapo kati yake 967 ni ya TAM na 735 ni ya ukaguzi wa mazingira.

Kadhalika alisema NEMC imetoa vibali 174 vya kushughulika na taka hatarishi nchini, vibali 10 vya kuingiza au kupitisha na kusafirisha nje ya nchi na kupeleka tani 516,041 za taka mbalimbali zilizokusanywa na kampuni zenye vibali.



## HABARI MBEYA

# Dk. Tulia atoa Shilingi mil.100 kwa wajasiriamali wanawake

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, ametoa Sh. milioni 100 kwa wanawake wajasiriamali 1,000 katika wilaya za Mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuwasaidia kukuza mitaji na kuendeleza biashara zao.

Alitoa fedha hizo juzi katika hafla iliyofanyika kwenye Uwanja wa CCM Rwanda Nzovwe ikiwa ni mwaka wa tatu mfululizo kugawa mitaji hiyo kwa wajasiriamali hao.

Alisema kati ya wanawake hao waliopatiwa mitaji hiyo, 750 ni kutoka Mbeya Mjini, 50 kutoka halmashauri zingine za mkoa huo.

Alisema anawasaidia wanawake hao ili wawe na uwezo wa kujimudu kiuchumi na kutumia mitaji hiyo kulea familia zao huku akisisitiza kuwa fedha hizo alizogawa ni msaada na siyo mikopo kwamba watatakiwa kurejesha.

Alisema alianza kugawa mitaji hiyo mwaka juzi kwa kuanza na wajasiriamali wa Jiji la Mbeya ambao aliwasaidia wanawake 400, mwaka jana wakawasaidia wanawake 600 na mwaka huu wanawake 1,000 na hivyo kufanya idadi kufikia 2,000.

Alisema kila mwaka wanawasaidia wajasiriamali tofauti na wanaokuwa wamenufaika kwa miaka mingine na kwamba hakuna mjasiriamali anayenufaika zaidi ya mara moja.

"Tutaendelea kuwafikilia wanawake kila mwaka kwa sababu tunaamini ukimwezesha mwanamke unakuwa umeiwezesha familia nzima, wanawake hawa wataitumia mitaji hii kushirikiana na kina baba kulea watoto," alisema Dk. Tulia.

Alisema baadhi ya wanawake hao wamekuwa wakikosa sifa za kukopesheka na halmashauri kutokana na kutokuwa na shughuli rasmi ambazo wanafanya na hivyo kwa kupewa mitaji hiyo watakuwa na nafasi ya kukopesheka.

Dk. Tulia alisema mbali na kuliwezesha kundi hilo pia kupitia taasisi yake ya Tulia Trust ataendelea kuyasaidia makundi mengine wakiwamo waendesha pikipiki za abiria na bajaji.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alimpongeza Dk. Tulia kwa kuwasaidia wajasiriamali hao huku akiwataka wanawake hao kuhakikisha wanazitumia fedha hizo kwa shughuli iliyokusudiwa badala ya kutapanya.

Alisema endapo watazitumia vizuri fedha hizo, watakuza mitaji yao na kubadilika kutoka kuwa wajasiriamali wadogo na kuwa wakubwa hali itakayowafanya wawe sehemu ya wachangiaji wa pato la taifa.

Malisa alisema Taasisi ya Tulia Trust imekuwa ikisaidia shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jiji la Mbeya ikiwamo huduma za afya na huduma elimu.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Wakili Triphonia Kisiga, alisema mitaji inayotolewa na Taasisi ya Tulia Trust inasaidia kukuza uchumi wa wananchi wa Jiji hilo na kuongeza pato la mwananchi.

Alisema halmashauri zote nchini zimekuwa zikitoa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wajasiriamali lakini fedha hizo huwa hazitoshi kutokana na wahitaji kuwa wengi zaidi.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, akiwaonyesha waandishi wa habari vipodozi vinavyodaiwa kuwa na viambata vya sumu, watu watatu walikamatwa wakiviingiza nchini kupitia njia za panya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ukosefu wa mizani chanzo wananchi kupunjwa ujazo gesi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IDADI kubwa ya wauzaji gesi ya kupikia katika Mkoa wa Mbeya, wamebainika wanafanya biashara hiyo bila kufuata masharti ikiwamo kukosa mizani hali inayosababisha ujazo pungufu kwenye mitungi.

Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Mbeya, Albogast Kajungu, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo kwa wafanyabiashara wa bidhaa hiyo.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara hao wanauza bidhaa hiyo kwa kuchanganya na bidhaa zingine jambo ambalo haliruhusiwi kwa mujibu wa sheria za biashara hiyo.

Alisema kutokana na matatizo hayo, viongozi wa WMA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), wameanza kutoa mafunzo maalumu kwa wauzaji wa nishati hiyo ili kuepusha madhara yanayoweza kutokana na biashara hiyo.

Alisema wananchi wamekuwa wakinunua gesi kwa bei kubwa lakini hawana uhakika wa ujazo.

Alisema mitungi imekuwa ikiandikwa ujazo lakini wananchi wanaponunua wanakuwa hawana uhakika na ujazo halisi uliomo kutokana na kukosekana kwa mizani na kwamba hali hiyo imekuwa ikisababisha wananchi kuibiwa.

"Ukipita huko mitaani unakuta mtu ana duka la kuuza bidhaa zingine lakini amewekewa mitungi kadhaa anaiuza nani ya kampuni tofauti tofauti, ukimuuliza mizani anakwambia yeye ni mjasiriamali mdogo, hii inasababisha malalamiko kuwa mengi," alisema Kajungu.

Alisema ili kukomesha hali hiyo EWURA wanatakiwa kuweka masharti ya uuzaji wa bidhaa hiyo na kuhakikisha yanasimamiwa vizuri ili kudhibiti uuzwaji holela wa bidhaa hiyo na kupunguza malalamiko.

Baadhi ya wajasiriamali wanaouza bidhaa hiyo walisema kampuni ya usambazaji wa gesi zimekuwa zikiruhusu kuuza bidhaa hiyo bila masharti yoyote jambo ambalo linachochea uuzwaji holela.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Happy Mwamajuja, alisema hakuna masharti yoyote ambayo wajasiriamali wanapewa wanapotaka kuanza kuuza bidhaa hiyo hali ambayo inasababisha wengi wawe wanaikimbilia.

Alisema wasambazaji wakubwa wa gesi hizo ndiyo wanaosababisha hali hiyo kutokana na wao kutaka kuuza bidhaa zao bila kuzingatia usalama wa watumiaji.

"Sisi wengine biashara zimeanza kufa kwa sababu kila mtu sasa anauza gesi, hakuna masharti yoyote kwa mtu anayetaka kufungua biashara hiyo, tunaomba serikali iweke utaratibu mzuri wa kudhibiti hali hiyo," alisema Happy.

Nao baadhi ya watumiaji wa bidhaa hiyo walidai kuwa wanauziwa gesi ambazo zina ujazo pungufu na hivyo kuwaingiza hasara kutokana na kuisha haraka.

Issa Mpili ambaye ni miongoni mwa watumiaji wa gesi alisema mbali na ujazo pungufu lakini wananchi wengi hawana elimu ya matumizi sahihi ya bidhaa hiyo hali ambayo inaweza kusababisha hatari.

Alisema baadhi ya mitungi inayotumika inakuwa imechakaa kwa kuliwa na kutu jambo ambalo linaweza likasababisha gesi kuanza kuvuja na kusababisha milipuko.

Mwakilishi wa Kitengo cha Malalamiko wa EWURA Mkoa wa Mbeya, Francis Mhina, alisema ofisi yake itaangalia namna sahihi ya kukabiliana na tatizo hilo ili kuhakikisha wananchi wanauziwa bidhaa sahihi.

# Watatu mbaroni tuhuma kuingiza vipodozi vyenye sumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kuingiza nchini shehena ya vipodozi vyenye viambata vya sumu ambavyo vimepigwa marufuku kutumika pamoja na vitenge kwa kupitia njia za panya.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, alisema majina ya watuhumiwa hao kwa sasa yanahifadhiwa kwa sababu za kiupelelezi ili kupata mtandao wa watu wengine wanaoshirikiana nao.

Alisema watu hao walikamatwa Machi 3, mwaka huu, katika eneo la Izumbwe nje kidogo ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi wakisafirisha shehena hizo kwa kupitia njia ya Ilembo-Mbalizi.

Alisema watuhumiwa walikuwa wanasafirisha shehena hizo kutoka katika nchi jirani ya Zambia kwa kutumia gari ndogo aina ya Creater GX 100 yenye namba za usajili T. 165 BQT.

Alisema watu hao walikamatwa kufuatia mtego maalumu uliokuwa umewekwa na makachero wa jeshi hilo baada ya kupata taarifa za siri kuhusu uwepo wa wasafirishaji hao wa bidhaa haramu.

"Kwa sasa upelelezi unaendelea kufanywa na makachero wetu wakiongozwa na Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai ili kuupata mtandao mzima lakini na kubaini mmiliki halali wa gari hiyo iliyokuwa inatumika," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema watafanya uchunguzi pia ili kubaini sababu za watu hao kutokamatwa walikotokea mpaka wakaenda kukamatwa mkoani Mbeya na kwamba endapo itabainika kuna maofisa pia wanashiriki kwenye shughuli hiyo haramu wataunganishwa kwenye kesi.

Alisema usafirishaji wa bidhaa hizo haramu una athari mbalimbali kwa taifa ikiwamo kuliingizia hasara kutokana na watu hao kukwepa kulipa ushuru lakini kuziweka afya za wananchi kwenye hatari kutokana na vipodozi vinavyoingizwa kuwa na viambata sumu.

Aliwataka wananchi kuacha kujihusisha na biashara hizo haramu kwa maelezo kuwa zina hasara kubwa kuliko faida hasa wanapokamatwa na vyombo vya dola.

Aliwataka pia wananchi mkoani humo kuendelea kutoa taarifa za siri kwa jeshi hilo kuhusu wahalifu ili vitendo hivyo vidhibitiwe kabla havijaleta madhara kwenye jamii.



# M/kiti Demokrasia Makini atumbuliwa kisa kutowajibika

Na Mwandishi Wetu

CHAMA cha Demokrasia Makini kimemsimamisha uongozi aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Mohamed Ali Abdulla, kwa sababu ya kushindwa kuwajibika, kutoshirikiana na viongozi wa kitaifa pamoja na wanachama.

Uamuzi huo ulitangazwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ameir Hassan Ameir baada ya kufanyika kwa kikao cha halmashauri ya chama hicho.

Ameir alisema chama hicho kimemteua Mwenyekiti wa chama hicho Zanzibar, Tabu Mussa Juma, kukaimu nafasi hiyo hadi utakapofanyika uchaguzi mwingine.

"Mkutano wa kawaida wa Halmashauri ya Chama cha Demokrasia Makini katika kikao chake umemsimamisha uongozi aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Mohamed Ali Abdulla kwa kushindwa kuwajibika," alisema.

Alisema chama hicho mikakati yake ni kuhakikisha kinavuna wanachama wengi katika kipindi hiki kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 pamoja na kushika dola.

Alisema mikakati ya chama hicho ni kufanya mikutano ya hadhara nchi nzima ambayo itazingatia taratibu zilizowekwa za kufanya mikutano ya kistaarabu yenye kuishauri serikali nini cha kufanya na siyo kuwashambulia viongozi kwa kauli za kejeli.

"Katika mkutano huu tumezungumza masuala ya kufanya mikutano ya hadhara baada ya serikali kuruhusu kufanyika ambapo tumejipanga kuyatumia majukwaa kwa ajili ya kuishauri serikali zetu na siyo kutoa kauli za kebehi na kudharau kazi kubwa iliyofanywa na viongozi waliopo madarakani," alisema.

Ameir alisema Chama cha Demokrasia Makini kinaunga mkono juhudi zinazochukuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika mikakati yake ya kujenga nchi na kukuza demokrasia katika mfumo wa vyama vingi.


Alisema miaka miwili ya Rais Dk. Samia ameonesha nia ya dhati ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar katika maridhiano ya kisiasa, huku akitekeleza miradi ya kimkakati ikiwamo ya miundombinu ya maji safi na salama na nishati ya umeme. "Chama cha Demokrasia Makini kinachukua nafasi hii kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan katika kutimiza miaka miwili ya uongozi wake ambapo amefanya mambo makubwa ikiwamo kuimarisha demokrasia ya mfumo wa vyama vingi na kuwaunganisha wananchi," alisema.

Kaimu Mwenyekiti wa chama hicho, Tabu Mussa Juma, alisema wamejipanga kurudi chini kwa wanachama wake kwa ajili ya kujiimarisha na kuwa imara kuingia katika duru za kisiasa nchini.

Alisema amekabidhiwa jukumu hilo huku akiamini kwamba anao uwezo mkubwa wa kujenga chama chenye kuleta ushindani wa kisiasa.

"Nimechaguliwa kushika wadhifa huu ambapo matumaini yangu makubwa kwamba tutajenga chama chenye kujiimarisha katika ushindani wa kisiasa," alisema.

Katibu mkuu wa chama hicho, Cecilia Augustino, alisema migogoro na mivutano katika chama hicho sasa imepata jawabu ambapo wamedhamiria kufanya kazi kwa umoja kwa maslahi makubwa ya chama na wanachama wake.



Wanafunzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST), wanaosoma Diploma ya Uhandisi wa Elektroniki na Mawasiliano mwaka wa tatu, wakifanya mtihani wa vitendo jinsi ya kutengeneza 'Monitor za Computer' (LCD-MONITER), ikiwa ni wiki ya mwisho ya mitihani ya semista ya kwanza katika Taasisi ya Karume. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wapewa siri ya kuwa mabilionea

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara, amewataka wanawake kuendelea na utayari wa kujitoa, kuwa na ushindani wa biashara ili kujiletea maendeleo.

Alitoa rai hiyo jana baada ya kuzindua maonyesho ya wanawake na watoa huduma ikiwa ni maadhimisho ya kuelekea Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema siri kubwa za wafanyabiashara wakubwa nchini waliopata mafanikio walianza na ujasiriamali mdogo, hivyo ni vyema nao kuendelea ili kufikia malengo yao waliyojiwekea.

Alisema Tanzania inaongozwa na Rais Samia ambaye ni mwanamke na ni miaka miwili tu ya uongozi wake mafanikio makubwa yamepatika, hivyo ana imani kubwa kuwa wanawake wanaweza kuleta maendeleo.

Aidha, aliwataka kuendelea kushirikiana kupiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, aliwapongeza wanawake wa Zanzibar kwa juhudi wanazozifanya kwa kujishughulisha na kazi mbalimbali kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.

Alisema tatizo kubwa la wajasiriamali wadogo ni kukosa masoko na ubora wa vifungashio ambavyo ni miongoni mwa njia za kutafuta masoko.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Usawa wa Kijinsia na Kuwainua Wanawake (UN-Women), Lucy Tesha, alisema kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ni kufanya tathmini ya wanawake juu ya maendeleo yaliofikiwa katika uchumi endelevu katika nchi na kuona haja ya kuwainua zaidi.

Akisoma risala ya wajasiriamali na watoa huduma, Mratibu wa Wanawake na Watoto, Mtumwa Ali, alisema maonyesho hayo yanaenda sambamba na Siku ya Wanawake Duniani ambayo yameleta kauli mbiu ya kujikita zaidi katika matumizi ya teknolojia ili kuleta usawa wa kijinsia.

Alisema bado wanawake wingi hasa wa vijijini hawana uwezo wa kutumia teknolojia, hivyo wameiomba serikali kuwapa mafunzo wajasiriamali hao ya matumizi ya teknolojia ili kuwa na uwezo wa kutumia teknolojia na kufanya miamala.

Alisema ukuaji wa uchumi unachangiwa pia na wajasiriamali hivyo kupatiwa mafunzo ya teknolojia kutasaidia kukua kwa uchumi wa nchi.

## Dk. Mwinyi ataka chombo kitakachowaunganisha matabibu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwapo kwa chombo kimoja cha Afrika Mashariki kwa maofisa tabibu itarahisisha wataalamu hao kuwa na sauti moja na kujulikana katika maeneo ya Afrika na duniani.

Aliyasema hayo jana katika hotuba yake iliyosomwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, wakati akifungua mkutano wa maofisa tabibu wa Afrika Mashariki na Kati.

Mkutano huo ulilenga kujadili changamoto na kubadilisha mawazo juu ya kada hiyo.

Dk. Mwinyi alisema licha ya kuwapo kwa maofisa, kuwa na umuhimu katika mambo ya afya lakini kumeonekana kuwa na changamoto kubwa ya kutojulikana tofauti na wauguzi na madaktari.

Alisema hivyo kuna kila sababu ya wadau hao kuwa kitu kimoja katika kujitangaza na kujulikana.

Alisema uamuzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) cha kuandaa mkutano huo wa kwanza kwa Afrika Mashariki na Kati kujadili utatoa fursa kwa maofisa tabibu wa Zanzibar kutambuliwa katika kazi zao.

Dk. Mwinyi alisema mkutano huo lazima ulenge kutambuliwa usawa wa ofisa yoyote wa afya kutoka nchi za Afrika Mashariki kufanya kazi sehemu yoyote Afrika Mashariki na duniani.

Alieleza kuwa Serikali ya Zanzibar itatoa ushirikiano katika maadhimio yatakayofikiwa ili malengo ya wataalamu hao yanafikiwa katika kutambuliwa watendaji hao katika fani yao hiyo.

Alisema serikali inathamini jitihada za maofisa tabibu kwa sababu inajua faida zake katika mambo ya afya na kazi wanazofanya.

Alisema wakati umefika kwa wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuendelea kushirikiana katika mambo mbalimbali ya kuleta umoja na ushirikiano wakati wote kwa faida ya nchi hizo.

Mkuu wa SUZA, Profesa Mhammed Haji Makame, alisema uamuzi wa mkutano wa kwanza wa Afrika Mashariki na Kati kufanyika Zanzibar ni kuona kwa namna gani maofisa afya hao na watendaji wengine wa kada hiyo kujulikana katika mataifa mbalimbali.

Alisema SUZA inataka kuona watendaji hao wanakuwa na jumuiya moja katika kujadili mambo yao na kutambulika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Rais wa Chama cha Maofisa Tabibu Afrika Mashariki (GACOPA), Ausstin Oduor, alisema mkutano huo unajadili namna gani ya kutatua changomoto za maofisa tabibu pamoja na kufanya kazi popote katika nchi za Afrika Mashariki.

Alisema hivi sasa hata kama mtendaji wa fani hiyo akienda Kenya hafahamiki wala hawezi kupata nafasi ya kazi kwa vile bado hakuna umoja na kujulikana katika fani hiyo.

Alisema katika kufikia malengo ya mkutano huo hivi sasa wanatarajia kuandaa rasimu ya katiba ili kujulikana Afrika Mashariki na Dunia. Rais wa GACOPA Tanzania, Innocent Somboi, alisema licha ya kuwapo kwa jumuiya hizo lakini bado kuna changamoto ya kujulikana kwa watendaji hao.

Alisema kuwapo kwa mikutano hiyo ya kujadili mafanikio na changamoto kunaenda kutoa fursa kwa watendaji hao kufanya kazi na kujulikana Afrika Mashariki.

# Asilimia 30 wanaoishi vijijini wagundulika kuwa na usubi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZAIDI ya asilimia 30 ya wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini wamegundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa wa usubi unaosababishwa na minyoo inayotoka kwenye nzi weusi wanaopatikana kwenye maporomoko ya mito.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa kampeni ya unyeshwaji wa dawa kwa ajili ya kinga tiba dhidi ya ugonjwa huo uliofanyika Halmashauri ya Njombe Mji.

Mratibu wa Programu ya Kudhibiti Usubi kutoka Wizara ya Afya, Dk. Clara Mwansesu, alisema ugonjwa huo unapatikana kwenye maeneo ya vyanzo vya maji yanayokwenda kwa kasi na baadhi ya vijiji vya Halmashauri ya Njombe Mji vimeonyesha kuwa viashiria vya ugonjwa huo.

"Wizara tulifanya utafiti mwaka jana, tuligundua maambukizi yako juu ambapo baadhi ya vijiji kulikuwa na maambukizi zaidi ya asilimia 30, hivyo serikali kupitia Wizara ya Afya tumeamua kuanzisha umezaji wa dawa za kinga tiba kwenye Halmashauri ya Njombe Mji ili kuwatibu wananchi walioathirika na wale ambao hawajapata madhara tuwakinge," alisema Dk. Mwansasu.

Alisema kwa awamu hii utolewaji dawa utafanyika kwenye halmashauri 14 nchini ingawa mara nyingi umekuwa ukifanywa kwenye halmashauri 29 ambazo zimeathirika na ugonjwa huo.

Alisema kwa Mkoa wa Njombe ni Halmashauri ya Njombe Mji, Morogoro kwenye halmashauri tisa na halmashauri zingine tano kutoka Mkoa wa Tanga.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema kulingana na utafiti uliofanyika, moja ya maeneo yalioathirika na ugonjwa wa usubi kwa zaidi ya kiwango cha kawaida ni Wilaya ya Njombe hasa Halmashauri ya Njombe Mji.

Alisema kutokana na hali hiyo, serikali kupitia Wizara ya Afya imeleta mpango wa kumeza dawa ambazo zitakwenda kuzuia na kutibu ugonjwa wa usubi.

"Ugonjwa huu una dalili mbalimbali kama ngozi kupauka, ngozi kutoka mabaka, mwasho na ngozi kuchakaa kwenye macho, lakini dawa hizi zinasaidia watu wenye upele, chawa na mapunye pia," alisema.

Aliongeza kulikuwapo na tatizo kwa Watanzania wanapoambiwa kitu wanadharau na kutaka kuona madhara, lakini ugonjwa wa usubi upo na umeathiri watu wengi.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Emmanuel George, alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi hawaugui na wanakuwa salama, ndiyo sababu ya kuletwa kwa dawa tiba hizo.

"Kuna watu hapa Njombe wameshaugua, lakini wengi hatukujua shida ni nini, kumbe ni usubi," alisema George.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Njombe Mji, Dk. Isaya Mwasubila, alisema utafiti uliofanyika ulibaini maambukizi makubwa kwenye maeneo manne ndani ya halmashauri hiyo ambayo ni Itipula asilimia 30, Igola (asilimia 11.22), Mji Mwema (asilimia 5.68) na Mamongolo (asilimia nne).

"Kulingana na ukubwa wa tatizo tunatakiwa kunywa kinga tiba mara mbili kwa mwaka nyumba kwa nyumba kwa kutumia wagawa dawa ngazi ya jamii ili kuepuka ulemavu wa kudumu na umaskini," alisema Mwasubila.



Meneja wa Benki ya Azania tawi la Lamadi, Muhidin Mjuvi (kulia), akikabidhi funguo za pikipiki kwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vincent Anney (wa pili kushoto) pamoja na Mbunge wa Bunda, Boniface Getere (kushoto). Benki ya Azania imetoa pikipiki 68 zenye thamani ya mil.184/- kwa vijana wa Bunda ili kuwawezesha kujiajiri kupitia mkopo wa masharti nafuu ujulikanao 'Jikwamue', mwishoni mwa wiki Mugeta wilayani Bunda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yakabidhi kisima

**Na Mauld Mmbaga**

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) limekabidhi mradi wa kisima cha maji kwenye Shule ya Msingi Nyani wilayani Kisarawe mkoani Pwani ikiwa ni jitihada za kurudisha sehemu ya faida zake kwa jamii.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi kisima hicho, Mkurugenzi wa Fedha wa TANESCO, Renata Ndege, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu, Maharage Chande, alisema licha ya kwamba kazi kubwa ya shirika ni kusambaza umeme, wanaijali jamii.

"Tumekuja kukabidhi kisima cha maji chenye thamani ya Sh. milioni 14, ambacho kitawasaidia wanafunzi na wanakijiji wa Nyani kuondokana na changamoto ya upatikanaji majisafi na salama waliyokuwa nayo kwa muda mrefu," alisema.

Mbali na kukabidhi kisima hicho, pia walipanda miti 100 kwenye eneo la Shule ya Msingi Nyani ikiwa ni mkakati wa TANESCO wa kutunza mazingira kwa faida ya wote.

"Sote tunafahamu umuhimu wa miti katika kuleta mvua ambazo kwa kiwango kikubwa huchangia kuwapo maji kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme nchini, hivyo tunachokifanya leo, kina uhusiano wa moja kwa moja na kuwapo umeme wa uhakika nchini," alifanua Ndege.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, matukio yote yanayofanyika ni mwendelezo kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, mwaka huu.

"Ndio sababu leo tumekuja wanawake wa TANESCO, hususan wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani kutekeleza shughuli hizi," alisema.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa mradi huo, Diwani wa Mfizi, Yadhamicas Nghondo, aliishukuru TANESCO kwa kuwakumbuka wanafunzi na wananchi hao ambao walikuwa hawana huduma ya maji safi na salama.

Alisema wananchi walikuwa wanachota maji Mto Ruvu umbali wa kilomita tano, jambo ambalo lilikuwa ni hatari hasa kwa wanawake na wasichana huku muda mwingi wa uzalishaji ukipotea.

## Wapatiwa matibabu macho bila malipo

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

TAASISI ya Lalji Foundation kwa kushirikiana na Lions Club District 411C pamoja na Rotary EClub ya Masaki, wametoa matibabu ya macho bila malipo kwa wakazi wa Kahama mkoani Shinyanga kupitia kambi maalum ya kusaidia watu wenye matatizo ya macho iliyofanyika kuanzia Machi 2 hadi 6 mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapo, Mratibu wa Taasisi ya Lalji Foundation, Judith Kahatano, alisema wamefurahi kushiriki kusaidia watu wenye uhitaji.

Alisema takribani watu 1,800 wamefanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu na miwani kwa waliokutwa na matatizo ya macho.

"Sisi Lalji Foundation tumefurahi kuwa hapa kushiriki hili kusaidia ndugu zetu Watanzania wenye matatizo ya macho. Wamefanyiwa uchunguzi wa macho na waliokutwa na matatizo makubwa ya macho yamefanyiwa upasuaji na wengine kupatia miwani pamoja na dawa," alisema Kahatano.

Mmoja wa wananchi waliojitokeza kwenye kambi hiyo, Shija Michael aliwashukuru Lalji Foundation, Lions Club District 411C na Rotary Club ya Masaki kwa kuwakumbuka watu wenye uhitaji na kuwataka Watanzania kuiga mifano ya wenzao katika kukumbuka wahitaji.

"Nilikuwa ninasumbuliwa na macho kwa muda mrefu, baada ya kusikia kuna matibabu ya bure kutoka kwa ndugu zetu hawa, nilifurahia sana. Nimetibiwa na kupatiwa miwani bure, ambayo itanisaidia katika shughuli zangu za kila siku.

"Ninawapongeza sana kwa hili na ninawaomba kampuni zingine zifanye kama hawa kuja mikoani kusaidia watu wenye uhitaji," alisema Michael.

Kambi hiyo maalum ya matibabu inafanyika wilayani Kahama mkoani Shinyanga kuanzia Machi 2 hadi 6 mwaka huu na wakazi wa mji huo wamejitokeza kupata huduma.



Jopo la madaktari wa macho wakimtibu macho mkazi wa Kahama wakati wa kambi ya matibabu bila malipo wilayani Kahama mkoani Shinyanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## HABARI KITAIFA

## WMA yatoa siku 14 kumaliza udanganyifu vipimo vya gesi

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKALA wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Lindi umewapa wafanyabiashara wanaouza mitungi ya gesi na majiko ya kupikia majumbani kuwa na mizani ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wateja.

Meneja wa vipimo mkoani humo, Andrew Mbwambo, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha kupeana elimu kati yao na wafanyabiashara hao Manispaa ya Lindi.

Alisema kuwa baada ya muda huo kupita, watendaji wa vipimo watapita kufanya ukaguzi na mfanyabiashara atakayekutwa anafanya shughuli hiyo bila kuwa na mizani, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria iliyowekwa na serikali.

"Kila muuza gesi ahakikishe anakuwa na mizani itakayotumika kupima uzito wa makasha ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wateja wenu," alisema Mbwambo.

Pia aliwashauri wauzaji hao kufungua matawi machache yenye vigezo, ikiwamo mizani itakayotumika kupima mitungi ya gesi wateja wanapofika kununua.

Alisema kuna idadi kubwa ya watu walioingia katika matumizi ya gesi, hivyo ni muhimu wauzaji kuboresha biashara zao kwa kupima ili wateja wafahamu kiwango kilichoko ni sahihi na kilichoandikwa juu ya mitungi.

Alisema wakala huo hutumia vyombo vya habari zikiwamo redio, runinga na magazeti kuelimisha jamii umuhimu wa matumizi ya gesi.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuwa mabalozi wazuri wa kuwaelimisha wenzao ambao hawakupata nafasi ya kuhudhuria kikao hicho.

Wakichangia hoja, wafanyabiashara hao kutoka Halmashauri ya Mtama na Manispaa ya Lindi, Daudi Makaba, Hassani Mkupete na Sifuani Samson, waliushauri wakala huo kuwa na utaratibu wa kutumia vyombo vya habari kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwa na mizani ili iwe na uelewa.

Walisema kitendo cha kukosa elimu kinachangia wauzaji wa mitungi ya gesi na majiko kutokuwa na uelewa mzuri na kusababisha malalamiko kati yao na wateja wanaofika kununua bidhaa hiyo.

# Kina cha maji Bwawa la Nyerere chafika mita 135

**Na Mwandishi Wetu**

UJAZAJI maji katika Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere umefikia mita za ujazo 135 kutoka usawa wa bahari ukitoka mita 71.5 za awali wakati Rais Samia Suluhu Hassan aliporuhusu maji kuanza kujaa Desemba 22, mwaka jana.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mhandisi Mkazi wa mradi huo, Lutengano Mwandambo, alibainisha hayo wakati akizungumza na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) uliotembelea mradi huo.

"Tunashukuru maendeleo ya mradi yanaenda vizuri. Mpaka kufikia mwishoni mwa Februari mwaka huu, mradi ulikuwa umefika asilimia 83.3 na utakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Mitambo wa TRC, Heriel Makange, aliyekuwa ameambatana na Meneja wa Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Umeme (SGR), walisema wamefurahishwa kuona kazi hiyo ambayo bwawa hilo litakwenda kuwa mkombozi kwenye upatikanaji wa nishati ya uhakika.

Akieleza umuhimu wa mradi wa JNHPP kwa TRC, Makange alisema kukamilika kwa mradi huo unaokwenda sambamba na reli ya SGR, kutasaidia kuendesha mitambo itakayotumika kwenye reli katika kuharakisha usafiri kwa Watanzania na kasi ya maendeleo nchini.

"Mradi huu ni mkubwa sana unaotekelezwa na serikali ya awamu ya sita kupitia TANESCO na hivyo tuna imani kubwa kukamilika kwake kutasaidia sana katika shughuli za uendeshaji mashine katika mradi wetu wa SGR na kukamilika kwa miradi hii kutaleta manufaa makubwa kwa taifa letu," alisema Makange.

Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa TANESCO, Elihuruma Ngowi, alitaja faida za kukamilika kwa mradi huo kuwa ni umeme wa uhakika, kuimarisha kilimo, uvuvi, utalii, miundombinu na usafirishaji.

Pia alisema utasaidia kuboresha huduma ya majisafi na salama ambayo yatawafikia wananchi na kuongeza kiasi cha upatikanaji wa huduma hiyo.




Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, akimsikiliza Meneja Maendeleo ya Biashara wa Benki ya NBC Arusha, Prince Moshi (kushoto), akielezea kuhusiana na huduma za benki hiyo mahususi kwa wanawake wakati alipotembelea banda la maonesho ya huduma za benki hiyo lililoko kwenye maonesho ya mkutano wa pili wa wanawake na vijana wafanyabiashara barani Afrika yanayofanyika jijini Arusha. Wengine ni pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mtandao wa Uwezeshaji Wanawake Tanzania (TAWEN), Florence Masunga (kulia) pamoja wafanyakazi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgodi wakunwa na utendaji wa Samia kuvutia uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imeeleza kuridhishwa na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan kuvutia wawekezaji na kuboresha sekta ya madini na kuifanya kampuni hiyo kuendelea kukua kila mwaka.

Pia imeahidi kuendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha lengo la mchango wa sekta ya madini kufikia asilimia 10 ya pato ghafi la taifa linafikiwa mwaka 2025, sasa ukiwa asilimia 9.2.

Makamu Rais wa Kampuni mama ya GGML, AngloGold Ashati - anayeshughulikia miradi endelevu Ghana na Tanzania, Simon Shayo, aliyasema hayo jana alipozungumza kwa niaba ya wadau wa sekta ya madini katika mdahalo wa miaka miwili ya Rais Samia madarakani.

Shayo alitolea mfano kuwa ripoti za karibuni kutoka Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta, na Gesi Asilia (TEITI) zinaonyesha GGML inachangia kati ya asilimia 30 na 40 ya mapato yote au dhahabu yote inayouzwa kwa sekta ya madini Tanzania.

"Kwetu hiyo ni faraja na hapa Geita tunaamini kwa kushirikiana na serikali ya mkoa na halmashauri yetu na wilaya zetu tunaweza kuufanya mgodi wetu ukazalisha zaidi na wakati wote mgodi uendelee kuzalisha zaidi ya wakia 500,000 kwa mwaka," alisema.

Kiongozi huyo alisema wanaamini sekta ya madini inaweza kuvuka malengo yaliyowekwa na serikali iwapo wawekezaji pamoja na wachimbaji wadogo wataendelea kujengewa mazingira bora ya uwekezaji.

"Tunaendelea kuiomba serikali chini ya uongozi wa Rais Samia kuendelea kutuwekea mazingira mazuri, tunaahidi kuongeza tija kwenye migodi yetu na sisi AngloGold Ashanti kupitia mgodi wetu wa GGML tunaamini wakati wote tutaendelea kuwa sehemu kubwa ya mafanikio hayo ya sekta ya madini," alisema.

Aliongeza kuwa kuwapo kwa GGML Tanzania, kunajitafsiri si tu kwenye uchimbaji wa dhahabu na ulipaji wa kodi, bali pia kwenye uwekezaji kwenye jamii.

"Tunu yetu kubwa ni kwamba jamii ionekane kunufaika kwa sisi kuwapo hapa, tumejitahidi kwa uwezo wetu tangu tumeanza uchimbaji mjini Geita mwaka 2000 kuwekeza kwenye jamii.

"Uwajibikaji wetu kwa jamii. Tangu mwaka 2017, tumewekeza kila mwaka kati ya Sh. bilioni 9.2 hadi bilioni 9.5 na mwaka huu tunaamini tutapata fursa ya kuunganisha mipango miwili ya mwaka 2022 na 2023 ambapo kwa Wilaya ya Geita peke yake tutawekeza kiasi cha Sh. bilioni 18.4," alisema.

Alibainisha kuwa uwajibikaji wa GGML kwa jamii unajitafsiri katika elimu, afya na kipato.

Aliiomba serikali kuendelea kuhakikisha wanachokifanya kwa jamii kinaongeza tija kusaidia serikali kupiga hatua zaidi kwenye huduma za jamii kwa wananchi wanaozunguka mgodi kunufaika.

Katika mdahalo huo, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela, alisema mkoa huo ndio namba moja kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu nchini.

Alisema kuwa kwa miaka miwili iliyopita, wachimbaji wadogo na wa kati wamezalisha kilo 13,000, sawa na tani 13.5 wakati migodi mikubwa kama GGML imezalisha kilo 35,000 sawa na tani 35.

"Mchango wetu katika kipindi cha miaka miwili unaonyesha kuwa ardhi ya mkoa huu ina thamani ya Sh. trilioni tano ambayo ni sawa na robo ya bajeti ya taifa," alifafanua.

Alisema kwa kipindi cha miaka miwili, zaidi ya Sh. bilioni 400 zimekusanywa kama mapato katika migodi inayochimba dhahabu Geita.

"Ukiangalia miaka ya nyuma hata asilimia 50 ya fedha ilikuwa haijafikiwa. Rais wetu amejenga mazingira uwekezaji, ametangaza nchi kimataifa na wawekezaji wanaweza kuja bila kuwa na hofu wala wasiwasi wowote," alisema.

# BOOMPLAY, HALOTEL ZARAHISISHA ZAIDI USIKILIZAJI MUZIKI KIDIJITALI

**Na Mwandishi Wetu**

Boomplay, App namba moja ya kusikiliza na kupakua muziki barani Afrika, imeshirikiana na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Halotel, kuzindua kifurushi cha 'Boomplay na Halotel' ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuendelea kurahisisha usikilizaji wa muziki kidijitali kwa Watanzania.

Akizungumza na mwandishi wetu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita, Meneja Mkuu wa Boomplay Tanzania, Natasha Stambuli, alisema ushirikiano huo unawapa fursa wateja wa Halotel kupata intaneti bila malipo na vifurushi vya kujiunga ili kusikiliza muziki bila kikomo wakiwa na uhuru wa kusikiliza maudhui ya kulipia Boomplay kwa bei iliyorahisishwa.

Alisema wateja wa Halotel wanaweza kupata vifurushi vya intaneti vya kila siku vya Sh. 500 na bonasi ya MB100, bando la wiki la Sh. 2,000 na bonasi ya MB300 pamoja na bando la kila mwezi la Sh. 6,000 na bonasi ya MB 500.

"Ushirikiano huu ni hatua nyingine muhimu katika azma yetu ya kuhakikisha muziki unapatikana kwa urahisi zaidi kwa Watanzania wote kupitia mamilioni ya wateja wa Halotel, naamini unatoa fursa nzuri ya kuwakaribisha wapenzi wa muziki karibu zaidi na nyimbo zao pendwa na maudhui mengine mengi yaliyomo kwenye App ya Boomplay," alisema Stambuli.

Akizungumzia ushirikiano huo, Mkurugenzi wa Biashara wa Halotel, Abdallah Salum, alisema,

wateja wanaweza kufurahia usikilizaji bila matangazo na upakuaji bila kikomo wa mamilioni ya nyimbo kutoka kwa wasanii wanaowapenda kupitia App ya Boomplay kwa bei iliyorahisishwa baada ya kununua vifurushi vya Halotel Boomplay na kwamba kwa wale ambao hawako kwenye mtandao huo wanaweza kupata laini za Halotel kwenye maduka yao yaliyoko nchi nzima na kupakua App hiyo ili kupata huduma.

"Kama moja ya watoa huduma wa intaneti yenye kasi zaidi nchini Tanzania, tunapenda kutumia fursa hii kuwapa wateja wetu vifurushi vya intaneti kwa bei nafuu kutoka mtandao wa Halotel ulioenea maeneo mengi nchini kwa kuwawezesha Watanzania kufurahia maisha ya kidijitali. Kupitia ushirikiano huu, wateja wetu sasa wanaweza kufurahia muziki wanaoupenda kupitia App ya Boomplay kwa kutumia vifurushi vinavyotoa thamani na urahisi.

"Watumiaji wa Boomplay Halotel, wanahimizwa kuboresha App yao ya Boomplay hadi toleo la hivi karibuni zaidi ili kufurahia matoleo mapya ya App," alisema.

Boomplay ni huduma ya kusikiliza na kupakua muziki iliyojikita barani Afrika ambayo ina mamilioni ya nyimbo, podkasti, video na habari za burudani.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Sunshine ya Kibaha, Abdulaziz Mwangi (kushoto), Jesse Machemba (katikati) wa St. Anne Marie Academy na Claud Mhagama wa Brilliant, wakishindana kula chapati wakati wa Bonanza la Rweikiza lililofanyika mwishoni mwa wiki St, Anne Marie Mbezi Kimara kwa Msuguri, Dar es Salaam. Lengo la bonanza hilo ilikuwa ni kuwapa zawadi wanafunzi waliopata daraja la kwanza kwenye mitihani ya kidato cha pili mwaka 2021 na 2022. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Airtel, Wizara Maliasili na Utalii zaunga mkono kazi za wasanii*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel imesema itaendelea kuunga mkono kazi za wasanii wa ndani kama njia mojawapo ya kuinua utalii pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dodoma mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Mawasiliano Airtel Tanzania, Beatrice Singano, wakati alipokutana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbas pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Filamu nchini, Dk. Kiagho Kilonzo.

"Airtel imejitolea kuleta bidhaa na huduma bunifu ambazo zinaendana na mahitaji pamoja na maisha ya kila siku ya wateja wetu, kwa sababu hiyo, tunaelewa kwamba wasanii pia ni wateja wetu na ndio sababu tuliamua kuzindua Televisheni Mtandao ya Airtel ijulikanayo kama Airtel TV App na kuwapatia wateja wetu burudani zaidi wakiwa popote hapa nchini.

"Tunaona ni kwa jinsi gani serikali imeweka juhudi kubwa kwenye kuhamasisha maliasili zetu kwa kupitia utalii. Juhudi hizi ndio sababu moja wapo ya Airtel kuzindua Televisheni Mtandao ya Airtel ili kuwapa fursa wasanii wetu jukwaa la kuonyesha kazi zao. Lengo letu ni kuendelea kuunga mkono wasanii wetu ili kuinua vipaji vyao na kuweza kukua kupitia kidigitali kukuza kazi zao," alisema Singano na kuongeza:

"Ni furaha yetu kwamba kwa kupitia njia hii ya kisasa ya Televesheni ya Mtandao ya Airtel App, itaweza kuongeza thamani ya kazi za wasanii wetu. Tutaendelea kufanya kazi na Bodi ya Filamu Tanzania, Basata na Cosota ili kuhakikisha kazi za wasanii wetu zinarudisha faida na kuifanya sekta ya burudani kuendelea kuwa chanzo cha uhakika cha ajira."

Kwa upande wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Abbas, aliwapongeza Airtel kwa kuendelea kuunga mkono wasanii wetu na kufafanua kuwa hiyo ni ishara tosha kwamba sekta ya burundani na hasa upande wa Bongo Movie inaendelea kukua. "Nachukua fursa hii kuwapongeza Airtel kwa juhudi zao za kuendelea kuunga mkono wasanii wa ndani na sana sana kwenye uzinduzi wa Televisheni Mtandao ya Airtel ijulikanayo kama Airtel TV App kwani kwa sasa wasanii wetu wanayo jukwaa la kuonyesha kazi zao na hivyo kuwafikia walengwa wao wengi pamoja na kuongeza kipato. "Naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba wasanii wetu kutumia hii fursa na kutengeneza kazi nyingi zaidi ambazo zitawavutia watazamaji wengi hapa Tanzania.

"Wizara ya Maliasili na Utalii itakuwa tayari kufanya kazi na wasanii ili kutumia vivutio vyetu vya utalii wakati wanatengeneza kazi zao. Hii itakuwa ni njia sahihi ya kuunga mkono juhudi za Rais wetu, Mama Samia ya kutangaza utalii wetu kwa kutumia Royal Tour. Na kwa sasa tukiwa na Airtel tuna uhakika sekta yetu ya burundani itazidi kukua," alisema Dk. Abbas.

## New Generation na ubingwa Zanzibar leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VINARA wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar, New Generation Queens, wamesema mchezo wao wa leo dhidi ya wapinzani wao, Warriors Queens, ndio utakaowapa ubingwa msimu huu.

Timu hizo zinakutana leo katika Uwanja wa Amaan majira ya saa nane mchana katika mwendelezo wa Ligi Kuu ya Wanawake ambayo inaelekea ukingoni.

New Generation imefikisha alama 27 huku wapinzani wao hao wakiwa na pointi 25 wakikamata nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo.

Katika mchezo huo endapo New Generation itafanikiwa kushinda, rasmi itatawaza kuwa bingwa ligi hiyo huku ikiwa na mchezo mmoja wa kukamilisha ratiba ya ligi hiyo wakati wapinzani wao, huo ndio mchezo wao, Warriors Queens hiyo ikiwa ni mechi yao ya mwisho msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa New Generation, Ahmad Bakari, alisema msimu huu timu hiyo haikutaka kufanya makosa kama ya msimu uliopita kwa kuupoteza ubingwa.

"Tunajua tunashuka dimbani kucheza mchezo mgumu na wenye maamuzi, mchezo huu ndio utakaotufanya tuwe mabingwa, hivyo lazima tuhakikishe tunashinda ili lengo letu litimie," alisema.

## St. Anne Marie yaibuka kidedea Bonanza la Rweikiza

**Na Mwandishi Wetu**

BONANZA la Rweikiza limehitimishwa siku ya Jumamosi huku timu za St. Anne Marie kidato cha nne wakiibugiza bao 1-0 timu ya St. Anne kidato cha sita.

Mashindano hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya Shule ya St. Anne Marie Academy, Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam na kuzishirikisha timu za Shule ya Brilliant, Sunshine ya Kibaha na mwenyeji, St. Anne Marie.

Timu za St. Anne O level na A Level zilizifunga timu zingine za Sunshine na Brilliant na kutinga fainali. Michezo mingine iliyochangamsha Bonanza hilo ni mashindano ya kula chapati ambapo mwanafunzi wa shule ya sekondari Sunshine, Abdulaziz Mwangi aliibuka kidedea.

Akizungumza kwenye mashindano hayo, Mkurugenzi wa shule hizo, Dk. Jasson Rweikiza, alisema waliamua kuandaa bonanza hilo kama motisha kwa wanafunzi zaidi ya 400 wa shule hizo waliopata daraja la kwanza kwenye mitihani ya kidato cha pili mwaka 2021 na 2022.

"Hili ni Bonanza la kusherehekea mafanikio tuliyoyapata mwaka jana na mwaka juzi mfululizo, wanafunzi wetu wa kidato cha pili walifanya vizuri sana na tukaona haitakuwa vema wala haki tukae kimya."

"Tumeona tutambue ufaulu huu mzuri kama motisha kwa wanafunzi wetu. Kufundisha na kufaulisha kwa kiwango hiki siyo kazi rahisi ni kama vita na ukishinda vita silazima ufanye sherehe," alisema Dk. Rweikiza.

## ZISIKUPITE

**GVARDIOL AWANIWA CITY**
MANCHESTER City inataka kumleta mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 21, kutoka RB Leipzig ikiwa watamuuza mlinzi wa Hispania, Aymeric Laporte, 28, ambaye anaivutia Klabu ya Paris St-Germain. (***Star***)

**SPURS NA DAU LA KANE**
KLABU ya Tottenham Hotspur inataka angalau pauni milioni 100 ikiwa watamuuza mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, ambaye amebakiza miezi 15 katika mkataba wake wa Spurs. (***Football Insider***)

**JONG BADO HATAKI**
KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, anasakwa na Manchester United, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, hataki kuondoka Barcelona. (***Guardian***)

**CAICEDO KUSAINI BRIGHTON**
KIUNGO wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo, huenda akatia saini mkataba mpya na Brighton, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, bado anatarajia kuwaniwa na klabu kubwa zaidi za Ligi Kuu msimu ujao. (***Telegraph***)

**RABIOT ATAJWA CITY**
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 27, ametambuliwa na Man City kuwa mbadala wa mchezaji wa kimataifa wa Ujerumani, Ilkay Gundogan, 32, ambaye amekuwa akihusishwa na Barcelona. Wachezaji wote wawili mkataba wao unamalizika msimu wa majira ya joto. (***Football Transfers***)

**FELIX KUBAKISHWA CHELSEA**
KLABU ya Chelsea inataka kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23, ambaye yuko hapo kwa mkopo kutoka Atletico Madrid. (***Mail***)

**BARCA YAMGOMEA KESSIE**
KIUNGO wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie, amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka Barcelona, lakini klabu hiyo ya Hispania haina nia ya kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. (***Sport***)

**FIRMINO APIGA KIMYA LIVER**
MSHAMBULIAJI wa Brazil, Roberto Firmino, hakuwa amezungumza na klabu nyingine yoyote kabla ya kuamua kuondoka Liverpool wakati mkataba wake utakapokamilika msimu wa majira ya joto, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. (***Football Insider***)

**LOFTUS-CHEEK ATAJWA MILAN**
KLABU ya AC Milan inamtaka kiungo wa kati wa Chelsea, Ruben Loftus-Cheek na italazimika kulipa euro milioni 25 ili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. (***Calciomercato***)

**RICE ANYATIWA CHELSEA**
KIUNGO wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 24, anawaniwa na Chelsea msimu wa majira ya joto. (***Fichajes***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SILVA AKARIBIA KUTUA KUKIPIGA RASMI BARCA

### ●●● Tayari City imemwambia watakubali dau lolote linalokuja ambalo litafikia mahitaji yao ya pauni milioni...

**MANCHESTER,** England

BERNARDO Silva anakaribia kuhamia Barcelona baada ya kuripotiwa kuwa Manchester City wametaja bei ya kiungo wao huyo wa kati.

**Silva mwenye umri wa miaka 28, yuko katika msimu wake wa sita na City, lakini baada ya mataji manne ya Ligi Kuu England na mabao 51 kwa klabu hiyo, hivi karibuni alizun gumza kuhusu matakwa yake ya kutaka changamoto mpya.**

Hiyo ni baada ya kuhusishwa kwa muda mrefu na madirisha mengi ya uhamisho na Klabu ya Barcelona ambayo imekuwa ikimwania.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno, ambaye alifunga dhidi ya Newcastle United Jumamosi, ana mkataba na klabu hiyo hadi mwaka 2025.

Lakini kwa mujibu wa BBC Sport, Man City wapo tayari kumuachia mchezaji huyo mwishoni mwa msimu huu kwa bei inayofaa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, City wamemwambia Silva kwamba watakubali dau lolote linalokuja ambalo litafikia mahitaji yao ya pauni milioni 57.5.

Barcelona wanafahamu vema maendeleo ya hivi punde na wanasemekana kufanya kila wawezalo katika miezi ijayo ili kuhakikisha sheria za kifedha zinawaruhusu kumsajili.

Hata hivyo, maslahi binafsi ya Silva yanaweza kuwa kikwazo kwa wababe hao wa Hispania.

Ripoti zinaonyesha City hapo awali ilikataa mpango wa Barcelona wa kutoa pauni milioni 62 ili kumsajili katika dirisha la Januari.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 499,
MECHI KALI
BRENTFORD
VERSUS
FULHAM
1 | 1.94
X | 3.45
2 | 3.50
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ARTETA: ARSENAL IMENIPA RAHA ISIYOELEZEKA

**LONDON,** England

MIKEL Arteta alisifu bao la ushindi la Reiss Nelson katika dakika ya 97 dhidi ya Bournemouth kama "wakati wa sauti kubwa na wenye hisia kali zaidi" kwenye Uwanja wa Emirates katika wakati wake kama kocha jambo ambalo linapaswa kuwapa Arsenal imani zaidi ya kuweza kushinda taji la Ligi Kuu England.

Arsenal walikuwa nyuma kwa mabao 2-0 kutokana na Philip Billing kufunga bao la pili baada ya Marcos Senesi kufunga la kwanza.

Hata hivyo, Thomas Partey alipunguza kwa nusu dakika ya 62 kabla ya Ben White kusawazisha dakika nane baadaye.

Katika fainali ya kishindo ambayo ilishuhudia Arsenal wakipiga mashuti 31, msimu wa juu katika Ligi Kuu, Nelson alipiga shuti kali kutoka ukingoni mwa 18 na kupata ushindi mnono na kuamsha shangwe za furaha.

Benchi la ufundi la Arsenal lilifurika uwanjani huku mashabiki wakikaa kwa muda mrefu baada ya filimbi ya mwisho kuishangilia timu yao wakati huu wakiendelea kuwaongoza Manchester City kwa pointi tano kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

"Labda ni wakati mkali na wa kimhemko zaidi ambao tumeishi pamoja," alisema Arteta, ambaye aliteuliwa kuwa kocha wa Arsenal Desemba 2019.

"Safari ambayo tumekuwa pamoja na jinsi mashabiki na wachezaji wanavyosonga pamoja. Kuongeza wakati huo, ni maalum sana."

Tangu kufungwa na Man City Februari 15, mwaka huu, Arsenal imeifunga Aston Villa, Leicester City, Everton na Bournemouth.

Walimpoteza Leandro Trossard kutokana na jeraha la kipindi cha kwanza Jumamosi, lakini Nelson alifunga bao lake la kwanza la ligi tangu Oktoba na kuendeleza mwendo wao wa ushindi.

"Kushinda mechi nne kwenye Ligi Kuu ni ngumu sana na tumefanya tatu kwa wiki, ambayo ni ngumu zaidi," alisema Arteta.

"Tumefanya kwa njia mbalimbali na hiyo inapaswa kuzalisha imani zaidi. Leo (juzi) mambo mengi yameenda kinyume na timu."

# Mbappe aweka rekodi mpya PSG

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amempita Edinson Cavani na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa Paris Saint-Germain baada ya kufunga dhidi ya Nantes, Jumamosi.

Mshambuliaji wa Uruguay, Cavani, aliifungia klabu hiyo mabao 200, akiipita rekodi ya Zlatan Ibrahimovic, lakini Mbappe sasa yuko mbele yake.

Bao lake la kuvunja rekodi lilikuja dakika za lala salama wakati PSG ikishinda mabao 4-2 dhidi ya Nantes kwenye Ligue 1 Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alijiunga na timu hiyo kutoka Monaco kwa mkataba wa mkopo wa awali mwaka 2017 kabla ya kusajiliwa kwa mkataba wa kudumu wa euro milioni 180 na ndiye anabakia kuwa mchezaji wa pili ghali zaidi wakati wote.

Alifunga mabao 21 katika msimu wake wa kwanza, lakini akafikia kiwango tofauti kabisa msimu wa 2018-19, akifunga 33 kwenye Ligue 1 pekee.

Mbappe ameendelea na hali kama hiyo tangu wakati huo, huku bao lake la 201 akifunga baada ya mechi 247 pekee - Cavani alifunga mabao 200 katika mechi 301.


Aliwasili PSG wakati wa dirisha moja la uhamisho na Neymar, huku usajili wa Lionel Messi wa mwaka 2021 ukileta jina lingine kubwa.

Bado Mbappe amekuwa mchezaji thabiti zaidi kati ya hao watatu, akiifanya PSG kupata mafanikio mara kwa mara kutokana na kukosekana kwa Neymar aliyekuwa majeruhi mara kwa mara kabla ya kuwasili kwa Messi.

Inaonekana bila shaka kwamba Mbappe atadumu kwa muda wa kutosha kuchukua rekodi ya muda wote ya mabao ya Ligue 1.

Mshambuliaji wa zamani wa Monaco, Reims, Tours na Toulon, Delio Onnis, anashikilia rekodi hiyo akiwa na mabao 299.

Ili kumzidi, Mbappe huenda akahitaji kukaa miaka kadhaa kwenye Ligue 1, na hilo linaonekana kutowezekana kutokana na uhusiano wa karibu kuendelea na mastaa kama hao huku Real Madrid ikionyesha nia.



HABARI MICHEZO

,870,280

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/03/23 | 22:45 | Huddersfield vs Bristol City | 2.54 | 3.14 | 2.64 |
| 02. 07/03/23 | 22:45 | Walsall vs Bradford City | 2.54 | 2.88 | 2.78 |
| 03. 07/03/23 | 22:45 | Cheltenham vs Lincoln | 2.48 | 3.20 | 2.65 |
| 04. 07/03/23 | 23:00 | Plymouth vs Derby | 2.70 | 3.25 | 2.42 |
| 05. 08/03/23 | 01:00 | Audax Italiano vs Universidad Catolica | 2.95 | 3.01 | 2.33 |
| 06. 08/03/23 | 01:00 | Tacuary Asuncion vs Club General Caballero Jlm | 2.47 | 3.37 | 2.52 |
| 07. 08/03/23 | 13:00 | Shonan Bellmare vs Urawa Red Diamonds | 2.40 | 3.05 | 2.55 |
| 08. 08/03/23 | 13:00 | Vissel Kobe vs Nagoya Grampus | 2.22 | 3.15 | 3.00 |
| 09. 08/03/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Consadole Sapporo | 2.51 | 3.27 | 2.53 |
| 10. 08/03/23 | 13:00 | Kyoto Sanga vs Gamba Osaka | 2.29 | 3.20 | 2.84 |
| 11. 08/03/23 | 13:00 | Kashiwa Reysol vs Kashima Antlers | 2.75 | 3.32 | 2.30 |
| 12. 08/03/23 | 16:30 | Liptovsky Mikulas vs MFK Skalica | 2.55 | 3.15 | 2.55 |
| 13. 08/03/23 | 18:00 | Ismaily SC vs Farco FC | 2.50 | 2.71 | 3.16 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 06/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2146 | Esteghlal Tehran vs Gol Gohar | 2.14 | 2.86 | 3.53 |
| 16:00 | 3246 | El Daklyeh vs Ghazl EL Mahallah | 2.37 | 2.97 | 3.07 |
| 16:00 | 5593 | Legetafo Legedadi vs Hawassa Kenema SC | 4.20 | 3.15 | 1.71 |
| 16:30 | 4594 | Kenkre FC vs Tiddim Road Athlectic Club | 3.44 | 3.49 | 1.88 |
| 17:00 | 1846 | Shirak Gyumri vs Ararat Yerevan | 2.95 | 2.85 | 2.44 |
| 17:00 | 2688 | AL Riyadh vs AL Arabi (SA) | 1.76 | 3.10 | 4.54 |
| 18:25 | 3779 | Al Qadisiyah vs AL Hazm | 4.06 | 2.93 | 1.91 |
| 18:45 | 5775 | AL Akhdood vs Hajer Club | 1.75 | 3.19 | 4.43 |
| 19:00 | 1421 | AEL Limassol vs Apollon Limassol | 3.12 | 3.22 | 2.23 |
| 19:00 | 5736 | Voluntari vs Argesul Pitesti | 2.00 | 3.24 | 3.55 |
| 19:00 | 5782 | Ethiopia Bunna SC vs Welayta Dicha FC | 2.24 | 2.80 | 3.37 |
| 20:00 | 1411 | FK Mladost Gat vs Radnicki Nis | 2.54 | 2.92 | 2.67 |
| 20:00 | 1531 | Kasimpasa vs Antalyaspor | 2.18 | 3.41 | 2.99 |
| 20:00 | 1660 | Apoel Nicosia vs Nea Salamis | 1.27 | 5.07 | 10.57 |
| 20:00 | 2762 | Sandecja vs OKS Odra Opole | 1.90 | 3.28 | 3.59 |
| 20:00 | 5192 | Sparta Prague B vs Slavia Prague B | 1.87 | 3.43 | 3.54 |
| 20:00 | 5821 | Baltika Kaliningrad vs Ska Energiya | 1.97 | 3.34 | 3.29 |
| 20:30 | 4193 | Panathinaikos vs Panetolikos | 1.25 | 5.17 | 12.67 |
| 20:30 | 4441 | Sassuolo vs Cremonese | 1.78 | 3.54 | 4.09 |
| 20:30 | 4725 | FC Martigues vs Red Star | 2.74 | 3.10 | 2.52 |
| 21:00 | 1044 | Waldhof Mannheim vs SV Elversberg | 2.90 | 3.49 | 2.23 |
| 21:00 | 1439 | Aalborg vs Midtjylland | 3.70 | 3.50 | 1.93 |
| 21:00 | 2522 | Diosgyori Vtk vs Gyirmot FC | 1.72 | 3.64 | 3.94 |
| 21:00 | 2617 | AIK Football vs Varbergs Bois | 1.32 | 4.88 | 7.27 |
| 21:00 | 3158 | Vasteras SK vs Ostersunds | 1.53 | 4.14 | 4.86 |
| 21:30 | 2246 | Sepsi Osk vs CFR Cluj | 2.52 | 3.08 | 2.72 |
| 21:30 | 5644 | Maccabi Haifa vs Hapoel Haifa | 1.25 | 5.03 | 8.83 |
| 22:00 | 2107 | Jong PSV vs NAC Breda | 2.52 | 3.34 | 2.50 |
| 22:00 | 5021 | De Graafschap vs Helmond Sport | 1.57 | 4.06 | 4.69 |
| 22:00 | 5478 | Jong Ajax vs FC Oss | 1.73 | 3.80 | 3.95 |
| 22:00 | 5529 | Jong AZ Alkmaar vs Willem II Tilburg | 4.27 | 3.69 | 1.70 |
| 22:00 | 5572 | Jong Utrecht vs Roda Kerkrade | 2.76 | 3.54 | 2.22 |
| 22:00 | 5837 | ADO Den Haag vs Heracles Almelo | 2.87 | 3.39 | 2.22 |
| 22:30 | 3573 | Pro Vercelli vs Vicenza | 3.35 | 3.14 | 2.20 |
| 22:30 | 5232 | Genoa vs Cosenza | 1.41 | 4.02 | 7.53 |
| 22:45 | 2483 | Bohemians FC vs Drogheda Utd | 1.58 | 3.70 | 4.83 |
| 22:45 | 3097 | Torino vs Bologna | 2.31 | 2.95 | 3.15 |
| 22:45 | 3205 | Caen vs Sochaux | 2.39 | 3.11 | 2.85 |
| 22:45 | 4361 | Sligo Rovers vs St Patricks | 2.87 | 3.13 | 2.26 |
| 22:45 | 5313 | UCD Dublin vs Derry City | 11.35 | 5.37 | 1.20 |
| 22:45 | 5485 | Dundalk FC vs Shelbourne | 1.94 | 3.24 | 3.49 |
| 23:00 | 2357 | Brentford vs Fulham | 1.94 | 3.45 | 3.50 |
| 23:00 | 2479 | Defensores Belgrano vs Guillermo Brown | 1.85 | 2.97 | 4.46 |
| 23:00 | 3061 | Shamrock Rovers vs Cork City | 1.42 | 4.00 | 6.35 |
| 23:00 | 4021 | Villarreal B vs Alaves | 3.45 | 3.20 | 2.05 |
| 23:00 | 4518 | Osasuna vs Celta Vigo | 2.69 | 2.94 | 2.64 |
| 23:00 | 4589 | Godoy Cruz vs Racing Club | 3.10 | 3.15 | 2.17 |
| 23:00 | 4982 | Arsenal Sarandi vs Belgrano Cordoba | 2.89 | 2.95 | 2.41 |
| 23:15 | 2666 | Casa Pia Atletico vs Pacos Ferreira | 2.00 | 3.11 | 3.81 |
| 23:30 | 4357 | Cusco FC vs Union Comercio | 1.45 | 4.06 | 5.76 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TIMU TATU ZA WANAWAKE ZATINGA NUSU BETIKA S4C

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI keshokutwa, Jumatano itakuwa ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya Betika Tanzania, imezindua ligi maalumu kwa wanawake kwa ajili ya kuadhimisha siku hiyo huku timu tatu zikitinga nusu fainali.

Timu hizo ni Espanyol Queens, Kopa G Queens na Coco Beach Queens ambazo zimetinga nusu fainali ya mashindano ya Betika Sodo 4 Climate (S4C), yanayoendelea kwenye fukwe za Coco jijini Dar es Salaam.

Mechi ya Wanahabari Queens dhidi ya Spark Queens Jumamosi ijayo, itaamua timu ya nne itakayotinga nusu fainali hiyo itakayoanza kupigwa Machi 18, mwaka huu.

Ofisa Habari wa Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya Betika Tanzania, Juvelinaus Rugambwa, alisema wameratibu mashindano hayo ambayo ni mahususi kwa ajili ya kuhamasisha utunzaji wa mazingira.

Alisema Jumamosi ilikuwa ni siku ya programu maalumu ya kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani itakayoadimishwa Machi 8, mwaka huu.

"Katika Sodo 4 Climate, Betika tumeweka pia Ligi ya Wanawake kwa lengo la kuwawezesha na kuendeleza vipaji vya soka kwa waliopo mtaani ambao hawajapata fursa hiyo kwingineko.

"Pia Sodo 4 Climate mbali na kuhamasisha utunzaji wa mazingira, inatoa elimu kwa wanawake kutumia fursa katika jamii kwa kufanya mambo yatakayowaingizia kipato binafsi bila kuwa tegemezi," alisema.

Kwa wanaume, timu zilizofuzu nusu fainali ya Sodo 4 Climate ni RC FC ambayo iliichapa mabao 3-1 Bodaboda Msasani, timu hiyo sasa itaungana na Coco Beach FC na Espanyol huku timu itakayoshinda Jumamosi ijayo kati ya Wanahabari FC au IPP Media FC, itaungana nazo kwenye nusu fainali Machi 18.

"Vilevile S4C ni amshaamsha za promosheni yetu ya Betika Mtoko wa Kibingwa inayoendelea kote nchini kwa mashabiki 100 kushinda nafasi ya kuishuhudia dabi ya watani wa jadi, Simba na Yanga Aprili 16, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kwa gharama za Betika.

"Ligi ya Betika S4C itafikia tamati wiki moja kabla ya mechi hiyo ya watani, ambayo washindi wetu wa msimu wa tano wa Betika Mtoko wa Kibingwa watakuja Dar es Salaam na kuhudumiwa kwa hadhi ya nyota tano kisha kuishuhudia dabi hiyo ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema.

Alisema kwenye Betika Mtoko wa Kibingwa ni rahisi kushinda, unachotakiwa ni kucheza na Betika kwa kuweka mkeka wa kuanzia Sh. 500 au zaidi kwenye beti tano.

"Hata kama mkeka utachanika, lakini unaingia moja kwa moja kwenye promosheni ya Mtoko wa Kibingwa ambayo inafanyika kwa msimu wa tano sasa, msimu huu ikitoa mabingwa 100," alisema.




Kikosi cha Kopa G Queens, ambacho kimeungana na Espanyol Queens na Coco Beach Queens kuwa timu zilizotangulia nusu fainali ya mashindano ya Betika Sodo 4 Climate (S4C), yanayoendelea katika Ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba yataja mbinu kuiua Vipers Lupaso

INATOKA UK 24

kujiweka katika nafasi nzuri katika kundi lao.

"Wachezaji wote wameshiriki mazoezi isipokuwa Kibu Denis ambaye amekuwa na programu yake chini ya uangalizi wa daktari kutokana na kupata maumivu katika mchezo wa mkondo wa kwanza uliopigwa Uganda.

Morali za wachezaji ipo juu, wanafanya jitihada kubwa mazoezini ili kulishawishi benchi la ufundi kuwapa nafasi katika mchezo wa Jumamne," alisema Ahmed.

Simba jana walizindua kampeni yao ya kuujaza Uwanja wa Mkapa katika mchezo huo, ambayo ilianza saa 4:30, asubuhi ikiongozwa na Meneja wa Idara ya Habari, Ahmed msafara ukianzia Magomeni Mikumi, kupitia Manzese, Mwananyamala hadi Ufukwe wa Coco, jijini Dar es Salaam, ambayo ilipewa jina la 'Wenye Nchi Beach Party'.

# Michezo

Nipashe

Jumatatu Machi 6, 2023





Silva akaribia kutua Barca

UKURASA 21

# Simba yataja mbinu kuiua Vipers Lupaso

## ●●● Kocha asema wachezaji wapo tayari, Phiri atajwa huku wakizindua kampeni kabambe ya kuujaza Uwanja wa Mkapa...

**Na Saada Akida**

WAKATI miamba ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, ikiendelea kuchanga hesabu zake za kuibuka na pointi tatu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, itakapoikaribisha Vipers ya Uganda kesho kwenye mechi ya marudiano ya hatua ya makundi, imetaja mbinu za kuweza kutimiza lengo hilo.

Kocha Mkuu wa Simba Robertinho Oliveira, amesema tayari ameandaa silaha zake vizuri huku akiwapa baadhi ya wachezaji majukumu maalum ya kuhakikisha wanapata pointi tatu katika mchezo huo baada ya ule wa awali ugenini kushinda 1-0.

Simba inahitaji kuvuna pointi tatu katika mchezo huo wa nyumbani ili kuweka matumaini yao sawa ya kutinga robo fainali ya michuano hiyo, wakati huu wakiwa nafasi ya tatu na pointi zao tatu nyuma ya vinara Raja Casablanca ya Morocco yenye alama tisa na Horoya ya Guinea ambayo imeshavuna pointi nne huku Vipers ikiburuza mkia na pointi yake moja.

Wapinzani hao wa Simba wanatarajia kutua nchini leo, tayari kwa ajili ya mchezo huo utakaopigwa kesho, Jumanne katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam majira ya saa 1:00 usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, alisema kikubwa wanachohitaji ni safu yao ya ulinzi kuimarika na kujitahidi kutoruhusu washambuliaji wa Vipers kupata nafasi ya kutikisa nyavu.

Alisema jambo lingine ni safu ya ushambuliaji kuhakikisha wanatumia vema kila nafasi wanazotengeneza katika mchezo huo lengo lao likiwa ni kutafuta ushindi na idadi nono ya mabao.

Kuhusu mshambuliaji Moses Phiri ambaye alikuwa na kiwango kizuri katika michuano hiyo kabla ya kuumia, Mgunda aliwatoa hofu mashabiki akisema suala la kuanza katika mchezo huo lipo chini ya benchi la ufundi kwa kuwa wachezaji wote wana ari na mechi hiyo.

"Suala la kuanza au kutoanza kwa mshambuliaji, Mosses Phiri hilo ni siri ya benchi la ufundi, kila mchezaji Simba yuko tayari kuitumikia timu, tayari wachezaji wanajua majukumu yao na kazi kubwa ni kuhakikisha tunapata ushindi," alisema kocha huyo Msaidizi wa Simba.

Wakati huo huo Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi cha Simba kinaendelea na mazoezi ya kujiandaa na mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers utakaopigwa kesho.

Alisema kikosi kimeingia kambini baada ya mazoezi ya juzi jioni ya kujiandaa na mchezo huo na kwamba hawahitaji chochote zaidi ya ushindi na kupata pointi tatu ili

INAENDELEA UK 23




Moses Phiri

## Yanga yaiandalia Bamako dozi nene

**Na Adam Fungamwango**

HUKU kikosi cha Real Bamako kutoka Mali kikiwasili nchini alfajiri ya kuamkia jana, Klabu ya Yanga imesema imeandaa dozi kubwa zaidi kwa timu hiyo kuliko hata ile iliyotoa kwa TP Mazembe ambayo walishinda mabao 3-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Februari 19, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Mashindano wa Klabu hiyo, Saad Kawemba, amesema maandalizi yote ya mechi ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika yamekamilika na sasa wanachosubiri Jumatano ambapo mechi hiyo itachezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, saa 1:00 usiku, ikiwa ni ya raundi ya nne ya Kundi D.

"Maandalizi yote ya mchezo huo yameshakamilika, mchezo ni Jumatano, wageni wetu wamewasili alfajiri ya leo (jana). Usiku wa Machi 8 kwa Mpaka, tunahitaji kuubadilisha kuwa wa furaha si kwa wanachama na mashabiki wa Yanga tu, bali kwa Watanzania wote. Tunataka tufanye zaidi ya vile tulivyofanya kwenye mechi dhidi ya TP Mazembe, tunachoomba ni watu kujitokeza kwa wingi," alisema Kawemba.

Yanga, iko nafasi ya pili kwenye msimamo wa kundi hilo kwa pointi nne, na iwapo itashinda itafikisha pointi saba sawa na vinara US Monastir ya Tunisia ambao siku hiyo watakuwa jijini Lubumbashi nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kuivaa TP Mazembe inayoshika nafasi ya tatu kwa pointi zake tatu.

Baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, viongozi na wachezaji wa timu hiyo wamesema wameamua kuwasili nchini mapema kwa ajili ya kuzoea hali ya hewa, pamoja na kupata muda zaidi wa maandalizi. Akizungumza kwa niaba ya wenzake, mchezaji Bourama Togola, alisema wamejiandaa kikamilifu, ingawa hawezi kusema moja kwa moja kama watashinda mechi hiyo.

"Tumejiandaa sana kwenye mechi hii, siwezi kusema tutashinda, tutatoa sare au tutafungwa, huu ni mpira, lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutashinda.

"Tumekuja mapema kwa sababu ya kuzoea hali ya hewa ya Tanzania, lakini pia kupata muda wa maandalizi ya mechi yenyewe kwa sababu umuhimu wa pointi tatu utatuongezea matumaini ya kusonga mbele kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hii," alisema mchezaji huyo ambaye angalau ana uwezo kidogo wa kuongea lugha ya Kingereza.

Jumapili iliyopita, Yanga ilifanikiwa kuidhibiti Real Bamako na kutoka sare bao 1-1, kwenye Uwanja wa 26 Mars nchini Mali.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >